SUPA JACKPOT
TZS. 1,144,172,464
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#

**Wahasibu** Korti Kuu mbaroni kwa tuhuma za wizi wa milioni 600 za mirathi

UKURASA 3



## TIMBER AIPA PIGO ARSENAL

UKURASA 22


# Nipashe

Ijumaa Agosti 18, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581406

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




# Bunge lashtuka mapato ya NHIF

UKURASA 2



UHABA WA DOLA

## ACT yataka BoT inunue mafuta, wachumi wadai mbinu za Kenya

UKURASA 19



# Mtaala mpya waja na umri mpya wa kuanza shule

UKURASA 2

UKURASA WA 4

### MAWAKILI WAOMBA RAIS KUINGILIA KATI SAKATA KINA SLAA



MWENYEKITI wa Jopo la Mawakili wanaowatetea, Philip Mwakilima, amemwomba...

UKURASA WA 4

### CRDB YATANGAZA MSHINDI WA TATU WA GARI KAMPENI YA SIMBANKING

BENKI ya CRDB imemkabidhi Robert Masala, mkazi wa Goba, wilayani Ubungo, Dar es Salaam, gari...



UKURASA WA 19

KESI DADA BILIONEA MSUYA

### SHAHIDI AONESHA NGUO YA NDANI YENYE DAMU

SHAHIDI namba 16 katika kesi ya mauaji ya Aneth Msuya, Sajenti...



MICHEZO SIMBA SC YAANZA NA KASI YA 4G UK.24 KATUNI UK.6



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan akiongoza kikao maalum cha Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM, Ikulu ya Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Bunge lashtuka mapato NHIF

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC), imeshtushwa na mapato ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF). Makusanyo ni madogo dhidi ya matumizi makubwa kwa miaka mitatu mfululizo.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Jerry Silaa amesema hali hiyo inatoa ishara kupitia kuporomoka mtaji wake wa uendeshaji. Mtaji umetoka Sh. trilioni moja hadi Sh. bilioni 700 kwa hesabu zilizofungwa Juni mwaka huu.

Baada ya kikao cha kamati hiyo na uongozi wa NHIF bungeni, jijini hapa jana, Silaa aliwaambia waandishi wa habari kuwa: "Katika hesabu walizofunga Juni 2023, wanaelekea kupata nakisi ya Sh. bilioni 152 na mali za mfuko zimekuwa zikipungua kutoka Sh. trilioni 1.2 hadi Sh. trilioni 1.09.

"Ukiangalia mwenendo wa mfuko unavyokwenda, haileti sura nzuri katika uhai wa mfuko."

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, kwa mwaka 2019/20, kulikuwa na nakisi ya Sh. bilioni 49; mwaka 2020/21, mfuko ulipata nakisi ya Sh. bilioni 109; na mwaka 2021/22, ukawa na nakisi ya Sh. bilioni 204.

Mwenyekiti huyo alifafanua mkakati wa serikali kuhusu maboresho bima hiyo inayokusudiwa kuufikia umma wote wa Watanzania, sheria yake ikipitishwa na Bunge, NHIF ndiyo itakuwa na jukumu la kusimamia utekelezaji wake.

"Ukiangalia mwenendo wake na jukumu itakalopewa, kwa sababu sasa hivi wana wanachama milioni 1.35 ambao wameongezeka kutoka milioni 1.05 kwa miaka hii miwili au mitatu, inaonyesha kama ufanisi unazidi kusinzia," alisema.

Mwenyekiti Silaa alifafanua kwamba kwa sasa kamati iko katika majadiliano ya kina, ikitarajia majumuisho yake yatawasilishwa Ofisi ya Spika wa Bunge kwa ajili ya kutafuta njia bora ya maboresho yatakayowasilishwa kama ushauri kwa serikali kuupa uhai wa fedha mfuko huo.


**THE COMPANIES ACT, CAP 212 (R.E 2002)**
**LEARNIT INSTITUTE OF BUSINESS AND TECHNOLOGY LIMITED**
**NOTICE OF RESOLUTION TO WIND UP THE COMPANY VOLUNTARILY BY MEMBERS**

**NOTICE** is hereby given to the general public that by special resolution dated **1ST DAY OF JULY, 2023**, it was resolved to wind up **LEARNIT INSTITUTE OF BUSINESS AND TECHNOLOGY LIMITED** (herein "the company") voluntarily by members.

**FURTHER NOTICE THAT** I, Allen Kimbelwa under the care of Adelphos (T) Limited was appointed for the purpose of winding up the company.

**TAKE NOTICE** that all the creditors are hereby requested to furnish the liquidator with full details of their claims against the company at the address below within fourteen days (14 days) from the date of this notice

Dated at Dar es Salaam this 2nd day of July,2023.

**THE LIQUIDATOR**
**ALLEN KIMBELWA**
**P.o Box 24011,**
**Sixth Floor Msasani Tower, Msasani.**
**Dar es Salaam.**


# Mitaala mipya yapendekeza umri kuanza shule upunguzwe

**Na Mwanahamisi Mussa,**
TUDARCo

RASIMU ya mtaala mpya wa elimu kuanzia shule ya awali, msingi, sekondari na ualimu inapendekeza umri wa kuanza shule kuwa miaka mitano.

Kwa mujibu wa rasimu hiyo, mwanafunzi atasoma madarasa sita huku katika ualimu, mkazo ukiwekwa kuimarisha ufundishaji kwa ajili ya kupata watanzania watakaojiajiri badala ya kusubiri kuajiriwa.

Rasimu hiyo iliyowekwa katika tovuti ya Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), ina mitaala na muhtasari ambao utaidhinishwa na kuanza kutumika baada ya Sera ya Elimu na Mafunzo kuidhinishwa na mamlaka husika.

Rasimu hiyo ambayo Nipashe imeona nakala yake, inapendekeza kwamba ngazi ya elimu ya awali, umri wa mtoto kuanza shule uwe miaka mitano na itatolewa kwa muda wa mwaka mmoja tu.

"Katika elimu ya awali mtoto atajifunza stadi za kusoma, kuandika na stadi za awali za kuhesabu, sayansi na matumizi ya Tekonolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA," inapendekezwa katika rasimu hiyo.

Vilevile, mtoto atajifunza kuthamini utamaduni wa jamii yake, imani, tunu za taifa na utunzaji wa afya na mazingira.

Katika elimu ya msingi, rasimu hiyo inapendekeza elimu itatolewa kwa muda wa miaka sita katika hatua mbili - ya kwanza itatolewa kwa muda wa miaka miwili na itajumuisha darasa la I na la II, lengo likiwa kujenga umahiri katika stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK).

Hatua ya pili itaanzia Darasa la III hadi la VI na italenga kuimarisha stadi za KKK pamoja na stadi nyingine za maisha, hivyo mwanafunzi ataanza Darasa la I akiwa na umri wa miaka sita na kumaliza Darasa la VI akiwa na umri wa miaka 11.

Kwa upande wa sekondari, rasimu inapendekeza kuzingatia ngazi zote za elimu ya sekondari ya chini ambayo mwanafunzi ataanza kuipata akiwa na miaka 12 kwa kusoma elimu ya jumla na elimu amali.

Elimu hiyo imegawanywa katika mikondo miwili - elimu ya jumla na elimu ya amali. Mwanafunzi atachagua mkondo kulingana na matakwa, uwezo na malengo yake maishani.

Mkondo wa elimu ya jumla umegawanyika katika michepuo 11 ambayo ni sayansi, kilimo, michezo, TEHAMA, biashara, muziki, sayansi ya jamii, sanaa, ushoni, chakula & lishe na lugha.

Kuanzia kidato cha kwanza, mwanafunzi atachagua masomo katika moja ya michepuo kulingana na matakwa, uwezo na malengo yake ya maisha.

"Licha ya masomo katika michepuo yao, wanafunzi wote wa mkondo wa elimu ya jumla watachagua masomo ya ziada yakiwamo ya mkondo wa elimu ya amali, kulingana na ratiba na uwezo wa shule husika," inabainishwa katika rasimu hiyo.

Katika elimu ya sekondari ya juu, rasimu inapendekeza mwanafunzi ataanza kidato cha V akiwa na umri wa miaka 16 na kuhitimu akiwa na miaka 17.

"Elimu ya sekondari, kidato cha V-VI imejikita kwenye masomo ya jumla yatakayotolewa katika tahasusi, ili kumwandaa mhitimu kujiunga na elimu ya juu.

Mwanafunzi atachagua tahasusi kulingana na matakwa yake, uwezo na malengo yake ya maisha.

Katika Rasimu hiyo ilieleza masomo ya lazima ambayo mwanafunzi anatakiwa kusoma ni mawasiliano ya kitaaluma, historia ya Tanzania na maadili pamoja na somo la Basic Applied Mathematics kwa michepuo ya sayansi.

"Pamoja na masomo ya tahasusi, mwanafunzi atachukua masomo mawili ya lazima ambayo ni Mawasiliano ya Kitaaluma na Historia ya Tanzania na Maadili. Mwanafunzi ambaye hasomi somo la Hisabati na ambaye anasoma masomo ya sayansi, uchumi na uhasibu atalazimika pia kusoma somo la Basic Applied Mathematics.

"Iwapo mwanafunzi atasoma somo la Additional Mathematics katika ngazi ya sekondari ya chini na kufaulu, hatalazimika kusoma somo la Basic Applied Mathematics.

Katika elimu ya ualimu, rasimu inapendekeza mabadiliko ya mitaala ya elimu ya ualimu kwa kuweka mtaala wa astashahada ya ukufunzi wa karakana au maabara-amali, mtaala wa elimu ya stashahada ya ualimu- elimu maalum, mtaala wa elimu ya stashahada ya ualimu elimu ya msingi na mtaala wa ualimu wa elimu ya awali.

HABARI KITAIFA

# Wahasibu Korti Kuu mbaroni tuhuma ubadhirifu mil. 600/-

**Na Hamisi Nasri,** MTWARA

MWEZI mmoja baada ya gazeti hili kuripoti kuhusu ufisadi wa Sh. milioni 695 za mirathi zilizowekwa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Mtwara inawashikilia wahasibu watatu wa Mahakama Kuu Kanda ya Mtwara kwa tuhuma za ubadhirifu wa fedha hizo zaidi ya Sh. milioni 600.

Jumbe Makoba, Kaimu Mkuu wa TAKUKURU mkoani Mtwara, aliwaambia waandishi wa habari jana mjini Mtwara kuwa katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita, walipata taarifa za fedha za mirathi zilizokuwa zinawahusu wanufaika ambao ndugu zao walishafariki dunia, kuwa zimefanyiwa ubadhirifu mahakamani huko.

Makoba alisema kufuatia uchunguzi wa kina uliofanywa na TAKUKURU, walibaini kwamba wahasibu hao (ambao majina yao hayajatajwa), wamehusika kufanya ubadhirifu wa fedha hizo za mirathi za wanufaika mbalimbali, ndiyo maana wakashikiliwa kwa tuhuma za ubadhirifu.

"Tunawashikilia wahasibu watatu ambao ni wafanyakazi wa Mahakama Kuu Kanda ya Mtwara... tuhuma zao hawa ni kufanya ubadhirifu wa fedha za mirathi zilizokuwa zinawahusu wanufaika wa mirathi ambao ndugu zao wameshatangulia mbele ya haki,"alisema Makoba.

Kaimu Mkuu huyo wa TAKUKURU alisema tayari wameshachunguza na kukamilisha uchunguzi wa fedha Sh. milioni 234 ambazo zimefujwa na wahasibu hao.

Kwa mujibu wa Makoba, TAKUKURU imeshapeleka majalada saba kwa DDP ili kuomba kibali cha kuwafikisha watuhumiwa hao mahakamani kwa ajili ya kujibu mashtaka.

Alisema TAKUKURU inaendelea na uchunguzi wa zaidi ya Sh. milioni 460 za mirathi ambazo zimetafunwa na watumishi, Ndani ya juma hili utakamilika na hatua zaidi kuchukuliwa.

Mwezi uliopita, Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Mtwara, Enock Ngailo, aliiambia Nipashe kuwa majalada 55 yaliwasilishwa ofisini kwake. Saba uchunguzi wake ulikuwa umekamilika. Mengine 48 watakamilisha mwishoni mwa mwezi huu.

"Katika kupitia majalada yote haya, tumebaini kiasi cha Sh. 695,574,257.16 (Sh. milioni 695.574) ambazo ziliwekwa katika akaunti ya Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mtwara kwa ajili ya kulipwa wategemezi wa mirathi, imefanyiwa ubadhirifu.

"Ubadhirifu huu umefanyika katika kipindi cha mwaka 2020 hadi 2022. Hii mahakama ina akaunti BoT ambayo ni ya kielektroniki.

Sasa kwa utaratibu ni kwamba fedha za mirathi zinaingia katika akaunti ya mahakama kutoka benki ambazo marehemu walikuwa wameweka fedha zao zinapaswa kulipwa kwa walengwa (wategemezi wa mirathi).

"Sasa, baadhi ya watumishi wa mahakama hasa idara ya uhasibu badala ya kuwalipa yatima na wajane fedha zao, wao walitengeneza wategemezi bandia na kisha kujilipa," alifafanua.

Naibu Msajili wa Mahakama ya Tanzania Kanda ya Mtwara, Fredrick Lukuna, alipotafutwa na Nipashe mwezi uliopita alisema hawezi kulizungumzia suala hilo kwa kuwa hana mamlaka ya kufanya hivyo.

Mtendaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Leornad Magacha, alikiri kuwa na dosari hiyo kiutendaji. Hatua zimechukuliwa, zikiwahusisha TAKUKURU.

**HOJA YA CAG**

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), aligusia fedha hizo.

CAG, Charles Kichere, anasema katika ripoti yake hiyo kuwa alibaini kutokuwapo rejista ya Akaunti ya Mirathi. Kanuni ya 131(1) ya Kanuni za Fedha za Umma za Mwaka 2001 (Toleo la mwaka 2004), inahitaji kiasi kilichopo katika akaunti moja moja za amana mwishoni mwa mwaka wa fedha kuorodheshwa na kufanyiwa usuluhisho na salio lililopo katika akaunti husika za udhibiti.

"Wakati wa ukaguzi wa Mahakama, nilibaini kuwa, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2021, Mahakama kama msimamizi wa mirathi, ilikuwa na jumla wa Sh. 26,656,717,909.04 (Sh. bilioni 26.657) katika akaunti ya mirathi iliyopo Benki Kuu.

"Hata hivyo, hakukua na rejista inayoonesha orodha ya wanufaika wa kiasi hicho; hivyo, usuluhisho wa rejista na akaunti ya benki haukuweza kufanyika kama inavyotakiwa na kanuni za fedha.

"Matokeo yake, ilikuwa vigumu kujua wanufaika wa fedha hizo za mirathi. Kutokana na hilo, ni maoni yangu kwamba menejimenti imekuwa na upungufu katika usimamizi wa fedha za mirathi zilizo chini ya uangalizi wa Mahakama," anabainisha.

CAG Kichere pia anasema aligundua ukosefu wa sheria na kanuni sahihi za usimamizi wa fedha hizo ni sababu ya upungufu huo na kutokana na kukosekana kwa usimamizi sahihi wa fedha hizo za mirathi, kunaziweka fedha hizo katika hatari za kutumiwa vibaya au akaunti hiyo kutumika kufanya miamala isiyoendana na lengo na madhumuni husika.

"Ninashauri Mtendaji Mkuu wa Mahakama kuhakikisha kwamba; kuna sheria na miongozo ya kifedha itakayoelekeza usimamizi wa fedha za mirathi na kuanzisha rejista ya mtandao ambayo itasajili wanufaika wote wa fedha hizo," CAG anawasilisha hoja yake.

# Watumishi JWTZ wadaiwa kuomba bilioni 1/- wamwachie waliyemteka

**Na Kulwa Mzee**

MTUMISHI wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Sufian Kideku na wenzake, wanadaiwa kuomba Sh. bilioni moja kwa ndugu wa Hussein Mohammed waliyemteka ili wamwachie.

Hayo yalidaiwa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam wakati washtakiwa hao wakisomewa mashtaka ya awali.

Mbali na Kideku, washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni mfanyabiashara Selestine Kamuli - mkazi wa Kizuka, Morogoro na Mtumishi wa JWTZ, Hussein Mwinyijuma - mkazi wa Gairo, Morogoro.

Wakili wa Serikali Happy Mwakanyamale, akisaidiana na Grace Mwanga, waliwasomea maelezo ya awali washtakiwa hao mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Ferdnand Kihwonde.

Wakili Happy alidai washtakiwa hao wanakabiliwa na mashitaka manne ambayo ni unyang'anyi wa kutumia silaha, kujitambulisha kama maofisa usalama, kuteka mtu kwa nia ya kumfungia na jaribio la unyang'anyi kwa vitisho.

Inadaiwa kuwa Mei 17, mwaka 2023, eneo la Zaramo Mtaa wa Jamhuri Posta, Ilala jijini Dar es Salaam, washtakiwa walijitambulisha kwa Hussein Mohammed kwamba ni maofisa usalama na walimtaka waende naye Kituo cha Polisi akahojiwe kuhusu tuhuma zinazomkabili.

Upande wa Jamhuri unadai Mohammed alikataa ndipo washtakiwa hao walimwibia simu aina ya iPhone na kumtishia kwa bastola aina ya Ruger huku wakimlazimisha aingie katika gari jeusi aina ya Toyota.

Inadaiwa kuwa washtakiwa walimfunga Mohammed kitambaa machoni na kuondoka naye kwenda eneo lisilojulikana. Wakiwa huko walitumia simu yake kupigia ndugu wa Mohammed wakaomba Sh. bilioni moja ndipo wamwachie.

"Ndugu baada ya kupewa maelezo hayo, waliomba msaada Jeshi la Polisi. Askari wa jeshi hilo walifanikiwa kuwakamata washtakiwa hao, hati ya ukamataji ilijazwa, washtakiwa walipelekwa Kituo cha Polisi Oysterbay na baadaye walifikishwa mahakamani.

Upande wa Jamhuri ulipomaliza kusoma maelezo ya awali, washtakiwa walikana yote isipokuwa majina, nyadhifa zao, mashtaka yanayowakabili na kufikishwa mahakamani.

Upande wa mashtaka unatarajia kuwa na jumla ya mashahidi 14 na vielelezo mbalimbali wakati wa usikilizwaji wa kesi hiyo.

Mahakama imeamuru shauri hilo kuanza kusikilizwa Agosti 25 mwaka huu.


## NOTISI / TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,YARDLEY RECOVERIES AUCTION LTD, SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya Benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| MBEYA | ROGIMWA AGRO COMPANY LIMITED | KIWANJA CHENYE HATI NAMBA 083KYL/1204 | ROGGERS GIDION MWAMENGO NA ANNA DANIEL SANGA | ITETE KYELA MBEYA | 22/08/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| DODOMA | ANOLD ANTONY MIKA | NYUMBA | ANOLD ANTHONY MICHAEL | NKUHUNGU DODOMA | 05/09/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | BERON CLASSIC WEAR | NYUMBA | NELSON BALTHAZAR MURISHI | NDACHI EXTENSION | 05/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | SAMWEL CHARLES LENJOLE | NYUMBA | SAMWEL CHARLES LENJOLE | CHINANGALI WEST-DODOMA | 06/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | STEVEN ALEX MANGESHO | NYUMBA | STEVEN ALEX MANGESHO | MTAA WA MATHIAS-MIYUJI DODOMA | 7/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | KELVIN COSTA LEONARD | PAGALE LA NYUMBA | ANTONETA HENERY KOSIMAS | MKONZE CHINYIKA-DODOMA | 8/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | PETER ODHIAMBO BOAZ | NYUMBA | PETER ODHIAMBO BOAZ | BAHI-DODOMA | 12/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja,Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu **No. 0715868000/0754497396**
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

# CRDB yatangaza mshindi wa tatu wa gari kampeni ya SimBanking

**Na Maria Seme**

BENKI ya CRDB imemkabidhi Robert Masala, mkazi wa Goba, wilayani Ubungo, Dar es Salaam, gari jipya aina ya Toyota Crown baada ya kuibuka mshindi katika awamu ya tatu ya kampeni ya Benki ni Simbanking.

Masala aliyeibuka kidedea kwa mwezi Julai anaungana na Jared Ojweke aliyekuwa mshindi wa gari Juni na Mayani Hassan aliyekuwa wa kwanza mwezi Mei mwaka huu.

Akieleza namna anavyoitumia huduma za SimBanking, Masala alisema jana kuwa amekuwa mteja wa Benki ya CRDB tangu mwaka 2005 na huduma hiyo imekuwa ikimsaidia kufanya miamala hasa ya biashara zake kwa urahisi na kwa wakati.

"Mimi ni mwajiriwa hapa Dar, lakini nina biashara Mwanza ambako ndiko nyumbani. Simbanking huwa inanisaidia sana katika usimamizi wa mapato na matumizi ya biashara.

"Kati ya mwezi Mei na Juni nilikuwa na miradi ninaikamilisha, hivyo nilitumia sana Simbanking nje ya utaratibu wa kawaida. Ninadhani hii imechangia kwa namna moja au nyingine mimi kushinda gari hili," alisema Masala.

Tangu alipofungua akaunti ya Benki ya CRDB, Masala ambaye ni baba wa watoto wawili, anasema amekuwa akitumia huduma za Simbanking tangu mwanzoni ilipokuwa ikitumia teknolojia ya USSD pekee kwa kubofya *150*03# mpaka ilipoanzishwa programu ya kidijitali ya SimBanking App ambayo anasema ni rahisi na ina ufanisi mkubwa.

Kwa waajiriwa wenzake, Masala anawashauri kuitumia Benki ya CRDB pamoja na Simbanking ili kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kushinda zawadi kemkem zinazotolewa kila mwezi kuanzia fedha taslimu, simu za mkononi hata gari hasa Toyota Crown linalotolewa kila mwezi na Vanguard atakalokabidhiwa mshindi wa jumla.

Kama ilivyokuwa kwa washindi waliomtangulia, Masala naye amekabidhiwa gari hilo lenye thamani ya Sh. milioni 20 likiwa limekatiwa bima kubwa na kujaziwa mafuta 'full tank'.

Akimkabidhi zawadi hiyo, Meneja wa Benki ya CRDB Kanda ya Mashariki, Badru Idd, alisema kwa hali ilivyo sasa, ni ngumu kuepuka uchumi wa kidijiti, hivyo Watanzania hawapaswi kubaki nyuma watumie huduma za Simbanking, jukwaa bora zaidi nchini na linaloongoza kwa kutumiwa kati ya programu za benki zilizopo. "Leo (jana) tunamtangaza Robert Masala aliyeibuka mshindi wa gari kwenye droo iliyochezeshwa tarehe 3 mwezi huu Agosti. Yeye ni mshindi wa tatu kuondoka na gari baada ya Jared Awando Ojweke wa hapa Dar es Salaam na Mayani Yahaya Hassan wa mkoani Dodoma kushinda miezi miwili iliyopita. Simbanking ni ya kila mtu, unaweza kumaliza mahitaji yako ukiwa mahali popote," alisema Idd.

Ikiwa benki kiongozi nchini, meneja huyo alisema Benki ya CRDB inahakikisha wakati wote inaboresha huduma zake ili kukidhi mahitaji ya wateja ikitambua kwamba matarajio yao yanabadilika kila siku. Hivi karibuni Benki ya CRDB ilizindua SimBanking App mpya ikiwa ni sehemu ya jitihada za benki katika kuboresha huduma na kuleta mapinduzi katika sekta ya fedha nchini.

SimBanking mpya imetengenezwa kwa muunganiko wa teknolojia za kisasa na za hali ya juu ikiwamo akili mnemba (Artificial intelligence), jambo linaloifanya kuwa na uwezo



Waziri Kivuli wa Nishati wa Chama cha ACT Wazalendo, Isihaka Mchinjita akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati akitoa mapendekezo ya kupambana na mfumko wa bei ya mafuta nchini. **PICHA: EMMALOVENESS GASTON**

# Mawakili waomba Rais kuingilia kati sakata la Dk. Slaa, wenzake

**Na Mwandishi Wetu,**
MBEYA

MWANASIASA mkongwe, Balozi Dk. Willibrod Slaa na wenzake wawili, wanaendelea kusota mahabusu katika Kituo Kikuu cha Polisi Jijini Mbeya bila kufikishwa mahakamani, ikiwa ni zaidi ya saa 100 tangu walipokamatwa.

Dk. Slaa na wenzake wawili ambao ni Wakili Boniface Mwabukusi na Mwanaharakati Mpaluka Nyagali, maarufu Mdude Chadema, wanashikiliwa na Jeshi la Polisi.

Viongozi hao walikamatwa katika maeneo tofauti tofauti ambapo Mwabukusi na Mdude walikamatwa mkoani Morogoro usiku wa kuamkia Jumamosi iliyopita huku Dk. Slaa akikamatwa Jumapili mkoani Dar es Salaam na wote walisafirishwa mpaka mkoani Mbeya.

Mawakili wa wanasiasa hao pamoja na wanaharakati wa haki za binadamu wamekuwa wanashinikiza watuhumiwa hao kufikishwa mahakamani ama kuachiwa huru kutokana na muda kupita wa kuendelea kushikiliwa na polisi.

Jana Mwenyekiti wa Jopo la mawakili wanaowatetea, Philip Mwakilima, alimwomba Rais Samia Suluhu Hassan kuingilia kati ili wateja wao waachiwe, akidai kuwa kwa sasa yeye pekee ndiye mwenye uwezo wa kulimaliza.

Alisema kitendo cha wanasiasa hao kuendelea kushikiliwa kinalichafua taifa kutokana na kukiuka misingi ya sheria na haki za binadamu.

Alisema, mmoja wa wateja wao hao ambaye ni Wakili Mwabukusi ni mgonjwa - ana mishono mingi mwilini na hastahili kuendelea kulala sakafuni. Wakili Mwakilima alisema kwa hali aliyonayo, alitakiwa kama kweli makosa yanayosemwa hayana dhamana, angepelekwa gerezani ambako kuna maeneo anayoweza kulala. Alisema Dk. Slaa kwa umri wake na mchango ambao ameutoa kwa taifa. Hastahili kulala kwenye mazingira ambayo analala kwa sasa.

"Mpaka sasa hatuelewi watapelekwa lini mahakamani, kauli pekee ambayo mimi ninayo ni kwamba tuendelee kuwa wavumilivu. Sasa tumwombe Rais Samia aingilie kati, jambo hili siyo zuri kwa taifa," alisema.

Wakili Mwakilima pia alidai kuna uwezekano baadhi ya washauri wa Rais wanampotosha kwa kumpatia taarifa ambazo siyo sahihi, hivyo kusababisha viongozi hao waendelee kusota mahabusu.

Alidai kuwa wateja wao wamebambikwa makosa. Hawana uwezo wa kutekeleza uhaini kama ambavyo wamezushiwa. Hawana uhusiano na vyombo vyovyote vya dola.

"Tunamwomba Rais aingilie kati kwa sababu yeye ndiye kiongozi wa wote, pamoja na tofauti ya itikadi zetu za kisiasa. Rais wetu sote ni mmoja na tunaamini hili jambo liko ndani ya uwezo wake," alisema Wakili Mwakilima.

Jana waandishi wa habari pamoja na baadhi ya wananchi ambao wanafuatilia sakata hilo, waliweka kambi katika viwanja vya Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mbeya kusubiri viongozi hao kupandishwa kizimbani, lakini hadi muda wa mahakama kufanya kazi unakwisha, hawakufikishwa mahakamani.

# NEC yatoa vibali elimu mpigakura

**Na Halfani Chusi**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imetoa vibali vya kutoa elimu ya mpigakura katika Uchaguzi Mdogo wa Ubunge wa Mbarali na kata sita za Tanzania Bara kwa asasi tatu za kiraia.

Taarifa ya Tume iliyotolewa jana, ikitiwa saini na Mkurugenzi wa uchaguzi wa NEC, Ramadhani Kailima, ilibainisha uamuzi huo umefikiwa baada ya tume kukutana katika kikao chake cha jijini Dodoma.

"Tume imefikia uamuzi huo kwa kuzingatia kifungu cha 4C cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura 343 na kanuni ya 3 ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020, inayoipa jukumu la kutoa elimu ya mpigakura nchi nzima, kuratibu na kusimamia taasisi na asasi za kiraia zinazotoa elimu hiyo," ilibainishwa katika taarifa hiyo ya NEC.

Kailima alizitaja asasi za kiraia zilizopata kibali cha kutoa elimu ya mpigakura na maeneo watakayotoa elimu hiyo kuwa ni Alpha and Omega Reconciliation and Peace Building (AREPEB), itakayotoa elimu Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali katika Jimbo la Mbarali, Umbrella of Women and Disabled Organisation (UWODO) itakayotoa elimu Halmashauri ya Wilaya ya Madaba katika Kata ya Mtyangimbole na Bright Child Development Tanzania (BRIGHT CHILD), itakayokwenda Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi katika Kata ya Mwaniko.

Tume hiyo pia imetoa kibali cha utazamaji kwa Asasi ya Kiraia ya Bridge Development Trust Organization (BRIDETO), ambayo iliomba kutazama uchaguzi mdogo katika Kata ya Mwaniko, Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi na Kata ya Nala, Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

Kailima alisema katika taarifa hiyo kuwa tume imefikia uamuzi huo wa kutoa kibali hicho kwa kuzingatia kanuni ya 16(5) ya Kanuni ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020.

Alisema katika utekelezaji wa jukumu la kutoa elimu ya mpigakura, asasi hizo zitapaswa kuzingatia Mwongozo wa Elimu ya Mpigakura wa Mwaka 2020 katika kipindi chote cha kutoa elimu hiyo katika uchaguzi mdogo.

Kwa mujibu wa ratiba ya uchaguzi mdogo iliyotolewa na tume, uteuzi wa wagombea katika uchaguzi huo utafanyika Agosti 19 na 20 mwaka huu. Baadaye kampeni zitaendelea hadi Septemba 18. Septemba 19 itakuwa siku ya uchaguzi.

"Tume inatumia fursa hii kuzipongeza asasi zote za kiraia zilizopata kibali cha kutoa elimu ya mpigakura na utazamaji wa uchaguzi, na ninazikumbusha kuzingatia sheria, kanuni, taratibu, miongozo na maelekezo ya tume katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yao," alisisitiza Kailima katika taarifa hiyo.

Kwa mujibu wa tume, vibali hivyo vitatumika kuanzia Agosti 18 hadi Septemba 18 mwaka huu. Ni vibali vya mwezi mmoja.

# MATANGAZO

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## MAOMBI YA KUONESHA NIA YA UTOAJI HUDUMA ZA USANIFU NA UTIAJI CHAPA WA VIFAA NA MIUNDOMBINU YA NDANI KWA AJILI YA EACOP KUMBUKUMBU NA. 00000338

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki ("EACOP LTD"), inaalika kampuni yenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia ya utoaji huduma za usanifu na utiaji chapa wa vifaa na miundombinu ya ndani kwa ajili ya Kampuni ya EACOP Ltd.

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili, kwa ajili ya kusafirisha mafuta ghafi katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale, katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka rasi ya Chongoleani, Mkoa waTanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 296 zitakuwa nchini Uganda na kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA**
EACOP inaendesha shughuli zake katika mikoa mbalimbali na hivyo itakuwa na ofisi katika mikoa hiyo. Kwa hiyo, EACOP Ltd inahitaji huduma za usanifu na utiaji chapa wa vifaa na miundombinu ya ndani kwa ajili ya ofisi zake zilizopo Dar es Salaam, Tanga, Dodoma, Singida, Kahama na Bukoba.

**Mtoa huduma anapaswa**
- Atawajibika kupendekeza mitindo ya chapa ya ofisi, ambayo inajumuisha michoro ya ukutani, alama na vipengele vingine vya chapa.
- Atapendekeza na kutoa sampuli za vifaa vinavyotumika kwa uwekaji chapa ili kuhakikisha kuwa vina ubora wa hali ya juu na ni rafiki wa mazingira.
- Atawajibika katika utekelezaji wa utaiji chapa, kuhakikisha kwamba inafanywa kwa wakati na kwa ufanisi.
- Ataweka msimamizi wa mradi mwadilifu ambaye atawajibika kusimamia mradi, na kuhakikisha kuwa mradi unakamilika ndani ya muda uliokubaliwa na ndani ya bajeti
- Atatoa mpango wa ukarabati wa vipengele vya uwekaji chapa, kuhakikisha kwamba vinakuwa katika hali nzuri wakati wote wa matumizi yake.
- Atazingatia kanuni zote za afya na usalama wakati wa utekelezaji wa shughuli za utiaji chapa.
- Atatoa bajeti kwa ajili ya mradi, ikionyesha gharama zote zinazohusiana na usanifu, utekelezaji na ukarabati wa chapa.
- Awe na timu ya ndani ya ubunifu ili kutayarisha, kuboresha na kusanifu kazi za utiaji chapa.
- Lazima aweze kufanya kazi kulingana na miongozo ya chapa ya EACOP na kujumuisha ujumbe na taarifa zinazohitajika.
- Anapaswa kuwa na mchakato madhubuti wa kudhibiti ubora ili kuhakikisha vipengele vya chapa vinakidhi viwango na sifa hitajika za EACOP.
- Anapaswa kuwa na dhamira endelevu na hivyo kutumia vifaa na mchakato wa utiaji chapa unaohifadhi mazingira.

**VIGEZO MUHIMU:**
**Kampuni au taasisi zinazoonesha nia zinakaribishwa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zifuatazo.**
- Uthibitisho wa uwezo wa kiufundi kama vile vifaa, miundo mbinu, na muundo wa timu
- Uzoefu uliothibitishwa wa kufanya kazi katika miradi mikubwa yenye mahitaji makubwa ya Uwekaji Chapa..
- Cheti cha usajili toka BRELA na leseni ya Biashara
- Uthibitisho wa kusajiliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha mlipa kodi cha mwaka wahivi karibuni.
- Waombaji wanasisitizwa sana kuhakikisha kuwa wamesajiliwa kwenye kanzidata ya EWURA (LSSP) ya Watoa Huduma za Ugavi wa Ndani, wakati wa kuwasilisha maombi ya kuonesha nia,
- Kukidhi Kanuni za watoa huduma wa ndani za mwaka 2017 na fasili ya Kampuni ya Ndani.
- Udhoefu wa kampuni, utendaji kazi na uwezo wa kampuni kutoa huduma iliyobainishwa hapo juu kwa kuzingatia viwango kitaifa na kimataifa.
- Uthibitisho wa wasifu wa wafanyakazi muhimu watakaohusika katika kutoa huduma za mradi ikijumuisha vyeti vyao, kiwango cha elimu, uzoefu na uwezo wa kutoa huduma husika.
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha taarifa za fedha ya miaka mitatu iliyopita.
- Ushahidi wa sera na Mifumo ya Usimamizi wa shirika la HSE, utaratibu na mchakato kwa mujibu wa viwango vinavyotumika vya ndani na Viwanda kwa kazi zinazofanana.
- Uthibitisho wa kupiga vita rushwa, ufisadi, kwa kuzingatia Haki za Binandamu.

Kampuni yenye nia, uwezo na rasilimali za kutosha kutekeleza shughuli zilizotajwa hapo juu zinakaribishwa kutuma maombi pamoja na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya **procurement.tz@eacop.com**, (ukubwa wa barua pepe usizidi **20Mb**). Maombi yatumwe kabla au mnamo tarehe **1 Septemba 2023 saa 11 jioni** saa za Afrika Mashariki. Kichwa cha Barua pepe kiwe **REQ-00000338- kutoa huduma za utiaji chapa wa vifaa na miundombinu ya ndani kwa ajili ya Kampuni ya EACOP Ltd**.
Mradi wa EACOP. Maombi yote ya kuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20
Maombi yote yawasilishwe kwa lugha ya Kiingereza.

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia kulingana na EOI hii na kisha kufanya tathmini kwa kutumia vigezo vya ndani ili kubaini makampuni yatakayojumuishwa kwenye orodha ya (Makampuni) ya awali yaliyokidhi vigezo. Makampuni yaliyofuzu hatua za awali pekee ndiyo yatakayopewa mwaliko wa zabuni, kwa kutia saini Mkataba wa Kutunza Siri (NDA), kama mwendelezo wa wito wa mchakato wa utoaji wa zabuni. Kampuni ya EACOP LTD inayo haki ya kufanya maamuzi yake ya kuchagua au kukataa kampuni na kuheshimu maamuzi yake pasipo kutoa sababu kwa kampuni husika

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## MAOMBI YA KUONESHA NIA YA UTOAJI WA HUDUMA YA UCHAPISHAJI WA IDADI KUBWA YA MACHAPISHO YENYE CHAPA YA KAMPUNI YA EACOP LTD. KUMBUKUMBU NA. 00000337

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki ("EACOP LTD"), inaalika kampuni yenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia ya kutoa Huduma ya Uchapishaji wa Idadi kubwa ya Machapisho yenye Chapa ya Kampuni ya EACOP ltd.

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili, kwa ajili ya kusafirisha mafuta ghafi katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale, katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka rasi ya Chongoleani, Mkoa waTanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 296 zitakuwa nchini Uganda na kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**
Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki ("EACOP LTD"), inaalika kampuni ya uchapaji yenye uzoefu wa kutosha kutoa Huduma ya uchapaji wa nyaraka mbalimbali kwa idadi kubwa na zenye ubora wa hali ya juu. Kampuni ya EACOP inaendesha shughuli zake uwandani na kupitia ofisi zake katika mikoa mbalimbali ya Tanzania, hivyo basi Kampuni ya EACOP inahitaji huduma mbalimbali za uchapaji kwa matumizi ya ofisi zake na uendeshaji wa shughuli mbalimbali za mikoani na ugavi wa machapisho yenye chapa ya Kampuni ya EACOP.

**Mtoa huduma anapaswa:**
- Kuwa na uwezo wa kutoa huduma ya machapisho yenye ubora wa hali ya juu kwa miradi yenye machapisho mengi. Hii inajumuisha, ikiwa ni pamoja na, uchapaji wa mabango, brosha, Mabango ya vitambaa, vipeperushi, stika, flaya, na vifaa vingine vya matangazo.
- Awe na uwezo wa kuwa vifaa kadhaa wa kadha ili kutoa fursa ya kampuni kuchagua kutoka vifaa hivyo, vifa hivyo ni kama vile karatasi, diski, kitambaa, na vitu vingine kulingana na mahitaji.
- Awe na timu ya ubunifu ya ndani ili kutengeneza, kurekebisha na kusanifu kazi za uchapishaji.
- Lazima aweze kufanya kazi kulingana na miongozo chapa ya EACOP na kujumuisha ujumbe na taarifa zinazohitajika.
- Awe na mchakato madhubuti wa kudhibiti ubora ili kuhakikisha kuwa, vifaa vilivyochapishwa vinakidhi viwango na sifa za EACOP.
- Awe na uwezo wa kufikisha bidhaa zilizokamilika katika maeneo mbalimbali kama inavyotakiwa na EACOP.
- Atawajibika kubadirisha kifaa chochote kilichochapishwa na kukuharibika kabla, wakati na baada ya muda mwafaka baada ya kukabidhi.
- EACOP inaweza kuagiza uchapaji baada ya saa za kazi na hata wakati wa likizo ambapo hakuna malipo ya ziada yatafanywa kwa mtoa huduma.
- Atapaswa kutoa bidhaa kikamilifu kulingana na mahitaji ya EACOP, EACOP itahifadhi haki ya kurejesha bidhaa zozote zilizochapishwa zisizofuata kanuni zilizowasilishwa na bila kulipa gharama zozote zinazohusiana.
- Anapaswa kuwa na dhamira endelevu na hivyo kutumia vifaa na mchakato wa uchapishaji unaohifadhi mazingira.
- Ni lazima aweze kufungasha bidhaa iliyokamilishwa kwa mujibu wa miongozo ya Afya na Usalama ya EACOP.

**VIGEZO MUHIMU:**
**Kampuni au taasisi zinazoonesha nia zinakaribishwa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zifuatazo.**
- Uthibitisho wa uwezo wa kiufundi kama vile vifaa, miundombinu, na muundo wa timu
- Uzoefu uliothibitishwa wa kufanya kazi katika miradi mikubwa yenye mahitaji makubwa ya Uwekaji Chapa.
- Uwezo wa kufunga au kusimamia usambazaji kwenye ukanda wa bomba pale inapohitajika, hususan katika mikoa ya Kagera, Geita, Tabora, Shinyanga, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga.
- Leseni ya Biashara.
- Cheti cha usajili toka BRELA
- Uthibitisho wa kusajiliwa na Mamlakaya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha mlipa kodi cha mwaka wa hivi karibuni.
- Waombaji wanasisitizwa sana kuhakikisha kuwa wamesajiliwa kwenye kanzidata ya EWURA (LSSP) ya Watoa Huduma za Ugavi wa Ndani, wakati wa kuwasilisha maombi ya kuonesha nia,
- Kukidhi Kanuni za watoa huduma wa ndani za mwaka 2017 na fasili ya Kampuni ya Ndani.
- Uthibitisho wa wasifu wa wafanyakazi mhimu watakaohusika katika kutoa huduma za mradi ikijumuisha vyeti vyao, kiwango cha elimu, uzoefu na uwezo wa kutoa huduma husika.
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha taarifa za fedha ya miaka mitatu iliyopita.
- Ushahidi wa sera na Mifumo ya Usimamizi wa shirika la HSE, utaratibu na mchakato kwa mujibu wa viwango vinavyotumika vya ndani na Viwanda kwa kazi zinazofanana.
- Uthibitisho wa kupiga vita rushwa, ufisadi, kwa kuzingatia Haki za Binandamu.

Kampuni yenye nia, uwezo na rasilimali za kutosha kutekeleza shughuli zilizotajwa hapo juu zinakaribishwa kutuma maombi pamoja na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya **procurement.tz@eacop.com**, (ukubwa wa barua pepe usizidi **20Mb**). Maombi yatumwe kabla au mnamo **tarehe 1 Septemba 2023 saa 11 jioni** saa za Afrika Mashariki. Kichwa cha Barua pepe kiwe **REQ-00000337 - kutoa huduma ya uchapaji kwa kiwango kikubwa na huduma za bidhaa zenye chapa**.
Mradi wa EACOP. Maombi yote ya kuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20
Maombi yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiingereza.

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na kampuni yenye nia kulingana na EOI hii na kisha kufanya tathmini kwa kutumia vigezo vya ndani ili kubaini kampuni zitakayojumuishwa kwenye orodha ya (Kampuni) za awali ziliyokidhi vigezo. Kampuni ziliyofuzu hatua za awali pekee ndiyo zitakayopewa mwaliko wa zabuni, kwa kutia saini Mkataba wa Kutunza Siri (NDA), kama mwendelezo wa wito wa mchakato wa utoaji wa zabuni. Kampuni ya EACOP LTD inayo haki ya kufanya maamuzi yake ya kuchagua au kukataa kampuni na kuheshimu maamuzi yake pasipo kutoa sababu kwa kampuni husika.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Balozi wa India nchini Tanzania ni mfano wa kuigwa

**BALOZI** wa India nchini Tanzania, Binaya Pradhan, anastahili pongezi kwa jitihada zake za kuitangaza nchi yake vilevile kwa kazi kubwa ya kukutanisha mabalozi wenzake, wafanyabiashara, taasisi mbalimbali na viongozi wa kiserikali katika shughuli mbali mbali zinazohusu nchi yake.

Mabalozi wanapochaguliwa kuwakilisha nchi zao nchi za nje wanakuwa ni wawakilishi wa serikali za nchi zao na pia wanasimama badala ya marais wao.

Tangu alipoteuliwa kuja Tanzania kuiwakilisha nchi yake, amekuwa akiandaa matukio mengi yanayowakutanisha watu wa kada tofauti na kupata fursa ya kufahamiana na kubadilisha uzoefu wa shughuli zao.

Kati ya shughuli ambazo balozi huyo huwakutanisha watu wa kada mbalimbali ni meli za kijeshi za nchini kwake zinapokuja nchini na watu kupata fursa ya kuitembelea na kujua historia ya meli hizo.

Ushiriki wa mabalozi wengine waliopo nchini katika shughuli zinazoandaliwa na balozi mwenzao ni kielelezo kuwa hata yeye hujitoa kushiriki katika matukio yanayoandaliwa na mabalozi wenzake.

Balozi huyo amekuwa akiwashirikisha Watanzania katika fursa mbalimbali za mafunzo nchini kwake na mara nyingi huwa zinalipiwa na serikali ya India.

Watanzania waliosoma nchini India wanaushuhuda wa kutosha kuhusu jitihada zinazofanywa na balozi huyo kuhakikisha anawakutanisha wanafunzi wote waliosoma nchini kwake na kujuana na kubadilisha uzoefu walioupata nchini humo.

Wakati India ikisherehekea miaka 77 ya uhuru wake, balozi huyo aliandaa matamasha mbalimbali kwa wiki nzima na kushirikisha watu wa kada mbalimbali.

Mabalozi wa nchi mbalimbali wanaoziwakilisha nchi zao nchini Tanzania hupata fursa ya kukutana kutokana na sherehe zinazoandaliwa na balozi huyo.

India imekuwa ikitoa msaada mkubwa katika sekta ya afya kutokana na ushirikiano mzuri uliopo baina ya nchi hizo mbili.

Watanzania wengi wanapopatwa na maradhi yanayoshindwa kutibika nchini huenda India kutokana na nchi hiyo kuwa na huduma na madaktari wazuri wa magonjwa mbalimbali yanayoshindikana kutibika nchini.

Kutokana na ushirikiano huo. Madaktari wa Kitanzania kwa kushirikiana na wa India wamesaidia kuokoa maisha ya watu wengi kwa kutibiwa hapa nchini na kuwapunguzia gharama kama wangekwenda kutibiwa nje ya nchi.


Katika sherehe za kuadhimisha miaka 77 ya uhuru wa India ambapo Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abadallah Uledi, alikuwa mgeni rasmi alisema wakati Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu alipofanya ziara nchini India hivi karibuni na kukutana na viongozi wa hospitali kubwa na maarufu ya Apollo na BLK, ambazo amezishawishi kuja kuwekeza Tanzania.

Waziri Uledi alisema taarifa walizonazo ni kuwa hospitali hizo nimeonyesha utayari wa kuja kuwekeza nchini Tanzania.

Kama hilo litafanikiwa basi Tanzania itakuwa imepiga hatua kubwa katika sekta ya afya, kwa sababu hata watu wa mataifa mengine waliokuwa wakienda India, sasa watakuwa wanakuja nchini kufuata matibabu na nchini kwa kupunguza umbali wa kwenda huko na nchi itaongeza mapato ya fedha za kigeni.

Balozi Pradhan ni mfano wa mabalozi wanaotakiwa kuigwa katika utendaji.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Kipaumbele chetu kinapokuwa tamaa ya fedha, vijana tujue tunaangukia hatarini

Na Anjella Mndolwa, TUDARCo

**VIJANA** wengi wamekuwa na tamaa ya kutaka fedha nyingi za haraka kwa njia zisizo halali na hata wanashindwa kuwajibika kwa umma, hali inayochangia kupatwa na matatizo makubwa, hali inayoleta hasara kwa taifa, kama haitashughulikiwa ipasavyo.

Baadhi ya vijana hadi sasa wameonyesha kuwa na hamu kubwa ya kutaka fedha za haraka, kwani ni hali inayotajwa inaweza kusababishwa na vigezo au visa mbalimbali kama shinikizo kutoka katika jamii, mazingira ya kiuchumi, au kutamani maisha bora.

Wengi hadi sasa wamekosa uaminifu, wengine wamekosa utii wa sheria, pia bidii na ubunifu wa kazi umebaki kuwa mdogo, hata kuchangia kuwapo tamaa na uroho wa kupata fedha nyingi za haraka kwa njia kama ya rushwa na ufisadi.

Hiyo imekuwa ikitokea kwa vijana wengi kujishughulisha katika biashara zisizo rasmi kama vile dawa za kulevya, ili kupata kipato cha haraka na wengine kujikuta wakiingia kwenye tabia ya wizi na uporaji.

Vijana wengi wanakosa uaminifu na kufikiri kuwa ndio njia rahisi ya kupata kipato cha haraka na kuona kusoma hakuna maana, kutokana na tamaa ya kuwa mtu fulani au kufanikiwa kwa njia rahisi.

Kuna tabia zinazotokana na kuiga kutoka kwa vijana wengine wanaowazunguka ambao wako katika jamii moja, hata wanajikuta wanaingia kwenye hizo tabia na kupoteza uadilifu wao kwa kiasi kikubwa.

**Wengi hadi sasa wamekosa uaminifu, wengine wamekosa utii wa sheria, pia bidii na ubunifu wa kazi umebaki kuwa mdogo, hata kuchangia kuwapo tamaa na uroho wa kupata fedha nyingi za haraka kwa njia kama ya rushwa na ufisadi.**

"Kuna kauli isemayo mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.' Hii ni kwa wazazi ambao hawana muda na makuzi kwa watoto wao na kusababisha kujiunga na makundi ambayo sio rafiki kwao. Kwani ukimkuza vizuri na mwenendo unaostahili kijana mambo mema ambayo umemfundisha atayashika.

Pia, inatokana na vijana wengi kuwa mtaani na kukosa kazi, kwa wale waliomaliza chuo na kukosa ajira na familia pia inamtegemea ni rahisi kujiingiza kwenye makundi, ili kupata fedha za haraka za kukidhi mahitaji yake ya kila siku.

Wito kwa serikali, kuwepo na mwongozo wa elimu ili kusaidia kuelewa umuhimu na kuwajengea msingi thabiti wa kifedha.

Vilevile, ni elimu inayotajwa itasaidia wanafunzi mashuleni ili kupunguza utegemezi wa ajira pindi wanapomaliza elimu na kutatua changamoto ya tatizo la ajira nchini.

Vilevile, viongozi ambao ni vijana, wanapaswa kuwa mfano mzuri wa kuigwa katika taifa ili kuleta kiu na shauku kwa vijana wengine wanaowatazama ili wawe chachu katika kulinda amani kwa kufanya yanayostahili kwa taifa letu.

Kwa ujumla, kunahitajika mihadhara ya kila mara kama vile makanisani, misikitini, na majukwaa ya siasa katika kujikita kwenye kutoa elimu ya uzalendo kwa vijana.



Kamishna wa Uhifadhi wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) Prof. Dos Santos Silayo akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma juzi, kuhusu utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya wakala huo katika kipindi cha miaka miwili ya serikali ya awamu ya sita. **PICHA: PAUL MABEJA**

# TFS yajipanga kuongeza tija uhifadhi, utalii

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KUTOKANA na juhudi zinazochukuliwa na serikali ikiwamo ubunifu wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan wa kuandaa filamu ya "Tanzania the Royal Tour" ambayo imetangaza nchi ndani na nje, Wakala wa Hifadhi za Misitu Tanzania (TFS), amejipanga kutumia fursa hiyo kuongeza tija katika uhifadhi, utalii na ukusanyaji maduhuli.

Kamishna wa Uhifadhi, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Profesa Dos Santos Silayo, alisema hayo jana jijini hapa, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa majukumu ya TFS kwa miaka miwili ya serikali.

"Juhudi zilizofanyika zimewezesha kuongezeka kwa idadi ya watalii waliotembelea vivutio vya utalii ikolojia ambapo hadi kufikia Juni 2023 jumla ya watalii 242,824 walitembelea vivutio hivyo," alisema.

Alisema idadi hiyo ni ongezeko la asilimia 60.8 ikilinganishwa na watalii 152,002 waliotembelea vivutio hivyo kwa kipindi hicho kwa mwaka 2021.

"Jumla ya Sh. 1,368,940,965 zilikusanywa ikilinganishwa na Sh. 603,311,740 zilizokusanywa mwaka uliopita ikiwa ni ongezeko la asilimia 126.9. Takwimu hizi zinaweka rekodi mpya kwani Wakala haukuwahi kufikia malengo haya hapo kabla," alisema.

Alisema katika kipindi cha mwaka jana TFS ilipewa fedha kiasi cha Sh. bilioni nne kutoka sehemu ya fedha alizotoa Rais kuboresha uhifadhi na shughuli za utalii katika misitu.

"Tumekamilisha kwa ufanisi ujenzi wa malango matano katika hifadhi tano, ujenzi wa barabara urefu kilomita 97 na njia za kutembea kwa miguu kilomita 190.5 katika hifadhi 11," alisema.

Aidha, alisema kupitia mpango kazi wa ndani wa taasisi TFS imeendeleza vivutio vya utalii wa kiikolojia na kiutamaduni kwa kukarabati kilomita 231.7 za njia za watalii na kilomita 643.54 za barabara za msituni na kuandaa ramani za vivutio vya kiikolojia katika misitu ya hifadhi.

Alisema Wakala pia umekamilisha ujenzi wa hosteli mbili moja katika msitu wa Wino, Songea na nyingine katika msitu wa SaoHill, Mafinga Iringa na kukarabati hosteli moja katika hifadhi ya Mazingira Asilia Amani.

Kadhalika, alisema kambi sita za watalii katika Hifadhi ya Mazingira Asilia Kilombero, Magamba na Mlima Hanang yamekamilishwa.

Vile vile, alisema wamejenga banda moja la kupumzika watalii, mageti matatu na mabango nane katika vituo vya Michoro ya Miambani Kolo - Kondoa na Magofu ya Tongoni - Tanga.

"Wakala umeendelea kutangaza vivutio vya utalii ikolojia, utamaduni pamoja na uhifadhi wa rasilimali za misitu kupitia maonesho mbalimbali ya ndani na nje ya nchi ikiwamo Sabasaba, Nanenane, Tanga Trade Fair, International Tourism Expo Japan 2022, East Africa International Tourism Expo, SITE na 2022 World Cup.

"Aidha wakala kwa kushirikiana na wadau uliandaa mashindano ya utalii maarufu kama West Kili Forest Tour Challenge, Bata Msituni Festival, na Sao Hill Forest Rally," alisema.

## Maofisa usalama feki wadaiwa kuomba bilioni moja kumwachia waliyemteka

**Na Kulwa Mzee**

MTUMISHI wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Sufian Kideku na wenzake, wanadaiwa kuomba Shilingi bilioni moja kwa ndugu wa Hussein Mohammed waliomteka ili wamuachie.

Hayo yalidaiwa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, wakati wakiwasomea maelezo ya awali washtakiwa hao.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni mfanyabiashara, Selestine Kamuli, mkazi wa Kizuka Morogoro na Mtumishi wa JWTZ, Hussein Mwinyijuma, mkazi wa Gairo, Morogoro.

Wakili wa Serikali, Happy Mwakanyamale, akisaidiana na Grace Mwanga, waliwasomea maelezo ya awali washtakiwa hao mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Ferdnand Kihwonde.

Wakili Happy alidai washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka manne ambayo ni unyang'anyi wa kutumia silaha, kujitambulisha kama ofisa usalama, kuteka mtu kwa nia ya kumfungia na jaribio la unyang'anyi kwa vitisho.

Imedaiwa Mei 17, mwaka 2023 eneo la Zaramo, Mtaa wa Jamhuri Posta, Ilala, Dar es Salaam, washtakiwa walijitambulisha kwa Hussein Mohammed, kwamba wao ni maofisa usalama na walimtaka waende naye kituo cha polisi akahojiwe kuhusu tuhuma zinazomkabili.

Upande wa Jamhuri unadai Mohammed alikataa na washtakiwa walimuibia simu na kumtishia kwa bastola huku wakimlazimisha aingie ndani ya gari jeusi.


Imedaiwa kuwa, washtakiwa walimfunga Mohammed kitambaa machoni na kuondoka naye eneo lisilojulikana na wakiwa huko walitumia simu yake kupigia ndugu wa Mohammed, wakiomba Shilingi bilioni moja wamuachie.

"Ndugu baada ya kupewa maelezo hayo, waliomba msaada Jeshi la Polisi, Polisi walifanikiwa kuwakamata washtakiwa hao, hati ya ukamataji ilijazwa, washtakiwa walipelekwa Kituo cha Polisi Oysterbay na baadaye walifikishwa mahakamani.

Upande wa Jamhuri ulimaliza kusoma maelezo ya awali, washtakiwa walikana yote isipokuwa majina na nyadhifa zao, mashtaka yanayowakabili na kufikishwa mahakamani.

Upande wa mashtaka unatarajia kuwa na jumla ya mashahidi 14 pamoja na vielelezo mbalimbali wakati wa usikilizwaji wa kesi hiyo. Mahakama imeamuru shauri hilo kuanza kusikilizwa Agosti 25, mwaka huu.

**KABWELA** — Na Fadhili Mohammed






Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Kinondoni, Ismail Seleman akizungumza na waandishi wa habari, Dar es Salaam juzi, kuhusu taarifa mbalimbali za utekelezaji katika kipindi cha miezi mitatu pamoja na ufuatiliaji wa mradi wa uboreshaji na upatikanaji wa huduma za maji wenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 65. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Muuguzi aliyedaiwa kubaka mjamzito aachiwa huru

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Wilaya ya Sikonge mkoani Tabora, imemuachia huru, Rayson Duwe, ambaye ni Ofisa Muuguzi daraja la pili katika hospitali ya wilaya hiyo aliyekuwa akikabiliwa na shtaka moja la ubakaji baada ya upande wa mashtaka kushindwa kuthibitisha tuhuma hizo.

Akitoa hukumu hiyo juzi, Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Wilaya ya Sikonge, Irene Lyatuu, alisema mahakama imepitia ushahidi wa pande zote mbili na kukosa uthibitisho unaomuweka hatiani ofisa huyo kuwa alimbaka mjamzito.

Alisema, upande wa Jamhuri ulitoa mashahidi saba akiwamo daktari, ushahidi ulioibua hoja zilizokinzana kuanzia tarehe na muda uliotendeka tukio hilo la ubakaji.

Alisema kuwa miongoni mwa mashahidi ni mjamzito ambaye alisema kuwa alibakwa Juni 10, majira ya saa tano usiku ikiwa ni siku ya pili baada ya kufika hospitalini hapo wakati akipatiwa huduma na ofisa muuguzi huyo, Rayson Duwe.

Alisema shahidi wa pili ambaye ni muuguzi, alidai tukio hilo lilitendeka Juni 9, majira ya saa mbili usiku huku shahidi wa tatu akidai tukio lilikuwa saa nne usiku ya Juni 9 hali inayofanya mashahidi wote kutothibitisha muda halisi.

Kutokana na maelezo hayo yaliyowasilishwa mahakamani na Hakimu Mwandamizi Lyatuu, akipitia kesi mbalimbali kulinganisha ili kupata uhalali wa kutoa maamuzi katika shauri hilo, alisema upande wa Jamhuri umeshindwa kuthibitisha tukio hilo na mahakama imemuachia huru ofisa muuguzi huyo kwa kuwa hakuwa na hatia iliyothibitishwa.

# USAID yatoa mil 74/- Taasisi ya Jane Goodall

**Na Jenifer Gilla**

MAREKANI kupitia Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Marekani (USAID), imeipatia Taasisi ya Jane Goodall Dola milioni 29.5 (Sh.milioni 74) kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Tumaini kupitia vitendo katika wilaya nne nchini kuhifadhi mazingira. Akizungumza katika hafla ya kusaini makubaliano ya utekelezaji wa mradi huo juzi, Dar es Salaam, Balozi wa Marekani nchini, Michael Battle, alisema wametoa fedha hizo zikasaidie jamii za Tanzania ili zinufaike na matunda ya uhifadhi wa rasilimali zao.

Mkurugenzi wa USAID Tanzania, Craig Hart, alisema fedha hizo ni mwendelezo wa ushirikiano na taasisi hiyo tangu mwaka 2003 kwa ajili ya kuhifadhi bayoanuai kwa kuziinua jamii zinazozunguka hifadhi hizo, ikiwamo ya Gombe ili mikakati yao iwe endelevu.

"Katikati ya ushirikiano tunalinda makazi ya sokwe takribani 500 ambao wapo hatarini kupotea kutokana na shughuli za ukataji miti zinazofanywa na binadamu, ili kukidhi mahitaji yao," alisema.

Alisema ni matarajio yake kuwa mradi huo utaboresha zaidi shughuli za uhifadhi na uzazi wa mpango, uwezeshaji wa kijinsia, hakiardhi, maendeleo ya kilimo pamoja na mabadiliko ya tabianchi.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Jane Goodall, Dk. Jane Goodall, alisema fedha hizo zitatumika kuhifadhi mazingira na kurudisha makazi ya sokwe kwa sababu bila kufanya hivyo viumbe hao wanaweza kutoweka.

Vile vile, zitasaidia watu wanaoishi mazingira duni, kutoa elimu kwa jamii na watoto kupenda na kulinda mazingira yao kwa kuwa kwa sasa uharibifu wa rasilimali unafanyika kwa kiwango cha juu.

"Tuna wafuasi kila sehemu, kuanzia ngazi ya shule za awali na katika vyuo vikuu na zaidi. Ni matumaini yangu kuwa vizazi hivi vitafanya mambo makubwa katika uhifadhi wa mazingira na bayoanuai hapo baadaye," alisema.

Alisema jamii zinashawishika kuharibu mazingira ili kukidhi mahitaji yao muhimu ikiwamo chakula, kuni kwa ajili ya kupikia, familia kama zikielimishwa na kupewa misaada ya kukidhi haja zao zinashiriki kuhifadhi mazingira na rasilimali zao.

Mkurugenzi wa Miradi na Sera wa Taasisi ya Jane Goodall Tanzania, Emmanuel Mtiti, alisema fedha hizo zinakwenda kutekelezwa katika wilaya za Dodoma, Uvinza, Tanganyika na Mpanda, kuzisaidia jamii hizo kuongeza kipato chao kupitia miradi ya akiba na kukopa.

Alisema watahamasisha uzazi wa mpango ili jamii ziwe na familia wanaweza kuzimudu, mpango wa elimu ya mazingira kwa watoto katika shule walioupa jina la 'roots and shoots', ili kuandaa kizazi kitakachotunza mazingira hapo baadaye.

"Lakini pia tutatengeneza mfumo wa kuangalia namna mazingira yanavyostawi katika ukanda wa Tanzania Magharibi. Tutaangalia namna mazingira yanavyoharibika na yanavyostawi katika ukanda huo," alisema.

Alisema pia watazisaidia jamii kutoka vijiji 104 kupata hati za ardhi za kimila ili kuhamasisha uhifadhi wa mazingira kwa kuwa wanaamini kuwa mtu akimiliki eneo anakuwa na mwamko mkubwa wa kulitunza.

# Madiwani watimua watumishi kwa kukiuka kanuni utumishi

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

BARAZA la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha limewafukuza kazi watumishi wawili kwa tuhuma za kukiuka kanuni za utumishi wa umma.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Erasto Makala, alisema hayo jana katika kikao cha baraza hilo cha kawaida kilichofanyika katika ofisi za halmashauri hiyo kuwa hatua hiyo ni moja ya kufikisha ujumbe kwa watumishi wasio waadilifu. Makala alisema waliofukuzwa kazi ni pamoja na Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Soga, Winnie Sambo, anayetuhumiwa kuhusika na upotevu wa vitabu 20 vya kukusanyia mapato.

Aidha Sambo anatuhumiwa kuhusika na upotevu wa fedha zaidi ya Shilingi milioni tatu ambazo zinadaiwa kutumika katika shughuli mbalimbali bila kufuata taratibu.

Mwingine ni Mwanaasha Yusuph, Ofisa Maendeleo ya Jamii, Kata ya Kwala, anayetuhumiwa kutumia zaidi ya Sh. milioni 28 ambazo zilikuwa ni marejesho ya mikopo ya vikundi.

Kwa mujibu wa Makala, ofisa huyo anadaiwa kutumia fedha hizo kwa ajili ya matibabu na ilitakiwa irejeshwe ili iingie kwenye mzunguko wa kuwezesha vikundi vingine kukopa.

"Hawa watumishi wameenda kinyume na kanuni ya Utumishi ya 42 ya mwaka 2022, tumelazimika kuchukua hatua hii kwakuwa hatupendi kuona mambo haya yanatokea kwenye halmashauri yetu kila mmoja anatakiwa kufanya kazi kwa kuzingatia kanuni na taratibu," alisema.

Awali, Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Butamo Ndalahwa, alisema wamejipanga kusimamia na kuchukua hatua maelekezo yote yaliyotolewa na Baraza la Madiwani.

Ndalahwa alisema hatua za kinidhamu na onyo dhidi ya watumishi waliotolewa maelekezo na baraza hilo yatafanyiwa kazi kuhakikisha kunakuwa na utendaji mzuri wa kuondoa kero za wananchi wanaowatumikia.

Moja ya maelekezo yaliyotolewa katika baraza hilo ni pamoja na Mkaguzi wa Ndani wa Hesabu za Serikali kufika kwenye vijiji kukagua matumizi na mapato.



# Vijana waonywa tabia ya kuunga mkono maandamano

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

MBUNGE wa Simanjiro mkoani Manyara, Christopher Ole Sendeka, amewakumbusha vijana kuepukana na suala la kuunga mkono maandamano ya kuipinga serikali yanayoendeshwa katika mitandao ya kijamii na baadhi ya watu wasioitakia mema nchi.

Alitoa rai hiyo wakati akizungumza kwenye kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, akitoa ushauri kwa vijana wa eneo hilo kutojiingiza katika kuunga mkono maandamano akisema ni sawa na kufanya uhaini.

Alisema serikali ina mkono mrefu katika kushughulikia amani iliyoko, hivyo aliwataka vijana wa eneo hilo wasijiingize kwenye uhasi au uhaini kwa kuwa watashughulikiwa.

"Ninampongeza Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Camillius Wambura, kwa kutoa onyo kupitia vyombo vya habari kuwa atawachukulia hatua watu au kikundi kitakachoandamana ili kuiangusha serikali kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025," alisema Ole Sendeka,".

Alisema endapo vijana watakuwa wanahitaji jambo lao ziko njia mbalimbali za kudai haki kupitia mazungumzo na mhimili mwingine ikiwamo Mahakama kuliko kuunga mkono maandamano ya uhaini.

"Hata kwenye makundi yenu ya mitandao ya kijamii msijaribu kuingia kwenye mtego wa kuwaunga mkono watu wanaotaka kufanya uhaini kwa kuwa mtachukuliwa hatua kali za kisheria na kisha kujuta baadaye," alisema Ole Sendeka.

Hata hivyo, aliwataka viongozi mbalimbali wa ngazi ya kata na vijiji, kuzungumza na vijana wa maeneo yao kuwa wasithubutu kuunga mkono uhaini unaofanywa kupitia mitandao ya kijami.

Alisema suala la uwekezaji wa bandari limefika hadi kwenye Mahakama hivyo ni jambo zuri na uamuzi umetolewa na endapo hawajaridhika wakate rufani na siyo kufanya uhaini wa maandamano.

"Unapotaka kuunga mkono au kufanya uhaini kwa serikali halali inayoongozwa na Rais Dk.Samia Suluhu Hassan utakuwa unajitafutia matatizo, hivyo vijana epukeni,"aliongeza Ole Sendeka.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Baraka Kanunga, alimuunga mkono mbunge huyo kwa kuwaasa vijana waepuke hayo na wafanye kazi ili kujiinua kiuchumi.

Alisema: "Vijana mnapaswa kujitambua na kuepuka kujiingiza kwenye mambo ambayo hayana maana kwa mustakabali wa taifa kwa kuwa suala la kuunga mkono uhaini litawagharimu," alisema Kanunga.



Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Dk. Suleiman Serera (kulia), akielezea taarifa ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi wa CCM 2020/2025 katika kipindi cha Januari hadi Juni 2023, kwenye kikao cha Halmashauri Kuu ya CCM Wilaya, mapema wiki hii. **PICHA: GIFT THADEY**

# Upatikanaji maji Simanjiro wafikia asilimia 58

**Na Allan Isack,** ARUSHA

KAIMU Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Simanjiro, Joanes Martine amesema hadi kufikia Juni mwaka huu hali ya upatikanaji wa maji wilayani hapa ni asilimia 58.6.

Amesema hali hiyo imetokana na kuchimbwa kwa visima virefu 76, visima vifupi 15, mabwawa madogo 28, mabwawa makubwa 15, chemchemu 12 na Mto Ruvu.

Aliyasema hayo wakati wa kikao cha baraza la madiwani na kusema wanatoa huduma kwenye kata 12 zenye vijiji 45 sawa na asilimia 72.6 ya wakazi wa wilayani humo.

Alisema kata za Mererani, Shambarai na Endiamtu, zinahudumiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha (AUWSA) na kata za Orkesumet, Edonyongijape na Langai, zinahudumiwa na mamlaka ya maji Orkesumet.

Pia, alisema wanaendelea kufanya matengenezo ya mara kwa mara katika maeneo yote pindi inapohitajika na kuhamasisha jamii kutunza vyanzo vya maji na mazingira.

Alisema wana changamoto ya upungufu wa maji kwenye vyanzo vya maji kwa ajili ya matumizi ya mifugo na binadamu na kuharibika kwa jenereta na mota za kusukuma maji mara kwa mara.

Naye Mbunge wa Simanjiro mkoani Manyara, Christopher Ole Sendeka na madiwani wa halmashauri ya wilaya hiyo, walipongeza uongozi wa RUWASA, kwa kufanikiwa kutoa huduma ya maji kwa wananchi wa eneo hilo. Ole Sendeka alisema RUWASA kupitia viongozi wake, Kaimu Meneja wa Wilaya ya Simanjiro, Joanes Martine na Meneja wa mkoa huo, Walter Kirita, wanastahili pongezi kutokana na utendaji kazi wao.

"Nawapongeza mno RUWASA ndiyo sababu hata bungeni niliwapongeza, Martine na bosi wake Kirita kwa namna wanavyotatua tatizo la maji kwa wananchi wetu,"alisema Ole Sendeka. Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Baraka Kanunga, alisema wakala hao wanastahili pongezi nyingi kwa namna wanavyotekeleza miradi hivyo.

Naye Diwani wa Kata ya Ngorika, Albert Msole, alisema Martine, amefanya kazi nzuri kwenye eneo hilo kupitia vyombo vya utoaji huduma ya maji ngazi ya jamii.

## Watakaovuruga amani mkoani Tanga kuchukuliwa hatua

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

SERIKALI mkoani Tanga imesema haitamvumilia mtu au kundi la watu watakaoingia mkoani hapa kwa lengo la kuvunja amani na utulivu, kwamba watachukuliwa hatua kali za kisheria

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba, alitoa angalizo hilo, wakati akifungua mkutano wa mafunzo ya matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 kwa viongozi, watendaji, wawakilishi wa vyama vya siasa na makundi maalumu mkoani hapa.

"Yeyote atakayekuja na wazo la kutaka kuvunja amani yetu katika mkoa huu akilianzisha sisi tutalimaliza kwa kuwa hatutaki taabu. Tunataka amani yetu iendelee na anayetaka shida aishie kwenye mipaka ya jirani asiingie katika mkoa wetu," alisema.

Alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wakufunzi kuchambua na kutumia matokeo ya sensa ili yatumike kuwa mwanzo wa dira ya kuwaongoza pamoja na utekelezaji wa majukumu na malengo yao ya kila siku.

"Mafunzo haya yatawajengea uwezo wa kutafsiri, kwa hiyo nawaomba sana wakati mafunzo yakiendelea kuweni watulivu ili yaweze kuwa msaada kwenye ngazi ya chini,"alisema.


Hata hivyo, alisema kwa mujibu wa takwimu ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, idadi ya watu mkoani hapa imeongezeka lakini siyo kwa idadi kubwa ya watu tofauti na mikoa mingine.

"Idadi yenu inaonesha kwamba kiwango chenu cha kuongezeka kimetoka asilimia 2.2 mwaka 2012 na kufikia asilimia 2.5 mwaka 2022, lakini pamoja na hayo, Mkoa wa Tanga unaonesha kwamba kasi yetu ya kukua iko chini sana ikilinganishwa na takwimu za sensa za kitaifa ambazo sasa ipo asilimia 3.2" alisema.

Meneja wa Takwimu Mkoa wa Tanga, Tonny Mwanyota, aliwaomba wadau wa sensa na wananchi kuwa wavumilivu kwa baadhi ya matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, kusubiria majibu ya matokeo kwa upande wa watu wenye ulemavu.

Mwanyota alisema matokeo ya sensa bado yanaendelea kutolewa kwa awamu, hivyo kwa ugumu wa takwimu kwa wenye ulemavu nayo ni miongoni mwa yale ambayo yanaendelea kufanyiwa kazi.

Alisema watu wengi wamekuwa wakiuliza sana kuhusiana na ripoti ya watu wenye ulemavu swali ambalo limekuwa likijirudia mara kwa mara.





# Meya atoa siku saba Soko la Mitumba kukamilika

**Na Aneth Ntungo,** SAUT

MSTAHIKI Meya wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza, Sima Constantine, ametoa siku saba kwa Ofisa Ugavi, Mhandisi Mkuu pamoja na Mchumi wa Halmashauri kuhakikisha wanatoa ushirikiano katika ujenzi wa vibada 45 vya machinga wa Soko la Mitumba Mlangommoja.

Alitoa atoa agizo hilo juzi alipotembalea na kukagua maendeleo ya wafanyabiashara hao ambao vibanda vyao viliungua kwa moto na kushangazwa na ujenzi wake kuendelea kudolola bila sababu za msingi.

Hivyo, aliwataka kumaliza changamoto zote ili ujenzi ukamilike na wapate maeneo rasmi ya kufanyia biashara zao.

Aidha, alisisitiza uwajibikaji baina ya wasimamizi wa ujenzi wa vibanda hivyo, kukemea uzembe unaoendelea akisema lengo likiwa ni kukamilisha miradi kwa wakati ili kuwasaidia wafanyabiashara kufanya shughuli zao katika maeneo yaliyo rasmi.

"Tukiendelea hivi ni sawa na kuwanyima fursa wananchi na vijana wenye nia ya kujiinua kiuchumi kupitia biashara zao na kuingizia kipato. Halmashauri hizi siku saba ziwatoshe kuhakikisha mnamaliza ujenzi ili waendelee na shughuli zao," alisema Sima.

Aidha, alieleza kuwa kuna watu waliokuwa wanapaswa kuingia katika vyumba hivyo zaidi ya miaka miwili, lakini mpaka sasa ujenzi haujakamilika na wanaendelea kuteseka kwa kukosa mahali sahihi ya kufanyia biashara zao.

"Pia nikuagize Ofisa Ugavi hakikisha vibanda hivi vikikamilika mnawapa kipaumbele wale waliokosa vyumba baada ya soko hili kuungua ili na wao waweze kupata maeneo rafiki kwa ajili ya shughuli zao,"alisema.

Mhandisi wa halmashauri anayesimamia mradi huo, Hakimu Albert alieleza kuwa lengo la mradi huo wa majengo matatu wenye maduka 45 ni kutatua tatizo la wafanyabiashara wadogo waweze kuwa na maeneo rasmi ya kufanyia shughuli zao. Alieleza kuwa mpaka sasa tayari umetumia zaidi ya Sh.milioni 180.9 na kueleza kuwa tatizo kubwa linalofanya mradi huo uendelee kuchelewa ni ucheleweshwaji wa vifaa kutoka kwa wazabuni wanaohitaji kulipwa kabla ya kuleta vifaa.



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maridhiano na Amani Wilaya ya Kahama, mkoani Shinyanga, Shekhe Amir Hassan (wa tatu kushoto), akizungumza na wajumbe wa kamati hiyo wakati wa usimikaji wa viongozi wa jumuiya, wilayani humo jana. Wengine ni viongozi mbalimbali wa jumuiya hiyo. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Wazazi wadaiwa kuwa chanzo watoto kufanyiana ukatili

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAZAZI wanaolala na watoto chumba kimoja wametajwa kuwa sababu ya wanafunzi wengi kufanyiana vitendo vya ukatili wa kingono wanapokuwa shuleni. Hayo yalibainishwa juzi na Mwalimu wa Shule ya Msingi Iselamagazi wilayani Shinyanga, Gatawa Donald, kwenye mkutano wa kuwasilisha matokeo ya utafiti dhidi ya kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia katika jamii wilayani Shinyanga, uliofanywa na Shirika la Citizen for change kwa ufadhili wa Mfuko wa Ruzuku Wanawake Tanzania (WFT-Trust).

Alisema wazazi wengi wamkuwa wakilala na watoto wao hususani wanaosoma madarasa ya awali na la kwanza wakidhani kuwa umri wao bado ni mdogo.

Alisema wanapofanya shughuli za faragha nyakati za usiku wanadhani kwamba watoto hao wanakuwa wamesinzia jambo ambalo siyo kweli.

Gatawa alisema watoto hao wanajifunza na kuanza kujaribu wanapokuwa shuleni hata mitaani, hali ambayo imekuwa ikiibua kesi za mara kwa mara.

Aidha, alisema baadhi ya watoto hao wamekuwa wakiwakamata shuleni wakifanya vitendo hivyo ikiwamo kushikana sehemu za siri, kwamba wanapowahoji wanaeleza kwamba wamemuona baba akimfanyia mama nyakati za usiku.

Mkuu wa Idara ya Ukuzaji Rasilimali na Mawasiliano kutoka 'WFT-Trust', Carol Mango, alisema jamii bado inahitaji kupewa elimu kuhusu vitendo vya ukatili pamoja na wazazi kuacha kulala chumba kimoja na watoto ambao tayari wameshajitambua.

Naye Mathias Mkude kutoka Citizen for change na TICD, akiwasilisha matokeo ya utafiti wa kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia wilayani Shinyanga, ambao wameufanya ndani ya miaka miwili kuanzia 2021-2023, alisema katika utafiti huo walitengeneza mbinu saba ambazo zitasaidia kutokomeza ukatili. Alizitaja mbinu hizo ni kufufua vikao vya familia nyakati za usiku za kabila la kisukuma (Shikome), kuhamasisha viongozi na walimu wakuu kuelimisha walimu kuhusu masuala ya ukatili, wanawake na watoto kuhudhuria kwenye mikutano ya kijiji na kutoa maoni yao dhidi ya kupambana na ukatili.

Mbinu zingine ni kutungwa sheria ndogo na kupitishwa adhabu kali kwa wazazi ambao watazuia watoto wao wa kike kwenda shule.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wilayani Shinyanga, Aisha Omary, aliipongeza WFT kwa kutoa ruzuku na kutekelezwa miradi ya kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia wilayani humo.

Alisema hali hiyo imesaidia kupunguza vitendo hivyo, huku wakiahidi wataendelea kuelimisha jamii juu ya malezi bora kwa watoto wao.

# Wahasibu wanawake watakiwa kutumia ujuzi kuinua uchumi

**Na Remmy Moka,** SAUT

WAZIRI wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amekikumbusha Chama cha Wanawake Wahasibu (TAWCA) kuwajibika katika kuchochea maendeleo ya nchi kwa kutumia ujuzi na maarifa stahiki kwa lengo la kuinua uchumi wa nchi.

Alitoa rai hiyo jana wakati akihutubia Kongamano la Uongozi wa Wanawake Wahasibu mwaka 2023, lililofanyika mkoani Mwanza na kuwataka kutambua kuwa wao ndiyo chachu ya maendeleo ya taifa.

Kadhalika, aliwataka kushirikiana katika utendaji kazi na kuzingatia mihimili mikuu ya utendaji kazi ambayo ni uzalendo wa taifa, uwajibikaji, uadilifu, utii pamoja na kuwa na hofu ya Mungu, kwani kwa kufanya hivi ndiyo nguvu ya mwanamke itaonekana

"Viongozi wanawake inabidi wapewe msaada ili waweze kufikia lengo lao na kuitekeleza mihimili mikuu ya utendaji kazi kama wahasibu wanawake nchini,"alisema DK.Mabula

Mwenyekiti wa TAWCA, Dk. Neema Kiule, alisema kuwa chama hicho kilianzishwa mwaka 2015, chini ya sheria ya jamii kikiwa na wanachama 18 lakini mpaka sasa kina wanachama 920.

Alisema chama hicho kimeendelea kufanya shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuelimisha jamii juu ya ujasiriamali, masuala ya pesa na kuwasaidia wanafunzi kuwa wataalamu wa uhasibu.

Alisema pia wamekuwa wakiwahamasisha wanawake na wanafunzi kupenda hesabu, kwamba kwa sasa wanapeleka vitabu vya hesabu na uchumi katika shule mbalimbali ili waweze kupata wahasibu wengi.



Ukurasa 12

Wakulima wanavyopaa kwa mradi kilimo cha kisasa wasimamizi ni wanahabari kinamama




Ukurasa 13

Ama kweli DP World imejua kutuvuruga Watanzania!



Ukurasa 14

## Wakulima wa Korosho katika neema mpya wakibangua kwa mashine zao


# BUFE

IJUMAA AGOSTI 18, 2023

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA


UCHUMI

### SAFARI YA 1961 HADI 2023

# Awamu ya Sita inavyoendeleza historia diplomasia uchumi Tanzania na China

**Na Mwandishi Wetu**

TANGU kupatikana uhuru wa nchi na kuanza kushuhudiwa mipango mirefu ya maendeleo miaka kadhaa baadaye, daima kumeshuhudiwa kihistoria kuwapo kwa wabia wa maendeleo, kulingana na mahitaji ya wakati.

Hata kabla ya miaka mitano ya maendeleo iliyoanza mwaka 1964 hadi 1969, nchini kumekuwa na wabia wa maendeleo kimataifa, mojawopo katika nafasi ya kipekee China na iliyokuwa Jamhuri ya Muungano wa Kisovieti (USSR).

Nchi hizo zilitoa fursa za kipekee, ikiwamo masomo ya kuzalisha wataalamu mataifa huru, watu wamekiwa na msaada mkubwa nchini.

Pia, katika lingine likabaki kuwa rekodi ya kihistoria ni mradi wa ujenzi wa reli ya Tanzania na Zambia, ikazaa shirika la reli linaloitwa TAZARA, kazi, iliyoanza mwishoni mwa miaka 1960, Mpango wa Maendeleo wa kwanza, 1964 hadi9 1969 unakamilika, ni mwingine akiwa Rais Kenneth Kaunda, ambayue taifa lake pia lilikuwa 'swahiba' wa Wachina.

Kupitia mustakabali huo, uhusiano huo umedumishwa ndani ya mapokezano ya awamu tofauti za uongozi nchini, sasa ikidumu awamu ya sita, taifa kama China limedumu kuwa rafiki, sasa uongozi wa nchi ukiwa katika awamu ya sita chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Katika staili hiyo iliyobeba zawadi ya kitaifa, Rais Dk. Samia amekuwa akiendeleza mustakabali huo wa kihistoria kukidhi



Barabara inayojengwa na kampuni ya Kichina nchini. **PICHA: MTANDAO**

mahitaji ya maendeleo ya Watanzania na marafiki wa kihistoria, hali kadhalika majirani wema.

Hiyo ikaanza na mwanzo wa nafasi yake ya kiuongozi, pale alipofanya ziara ndefu kwa mataifa marafiki ambao si wageni katika uhusiano na Watanzania kuanzia ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini, vilevile kwa ukanda wa ughaibuni, ikiwa na matokeo kadhaa au kimaendeleo yanayoshuhudiwa sasa.

Moja ya hatua ya mwendelezo wa hayo ya historia ya kimaendeleo, kukidhi mahitaji hayo ya kihistoria kati ya Tanzania na China, inaangukia katika mradi mkubwa wa sasa kujenga kituo kikubwa cha biashara, ikiwa na sehemu ya kupokea na kusafirisha bidhaa kati ya Tanzania na China.

Mradi huo ambao majengo yake yanaendeleza kujenga ilikokuwa Kituo cha Mabasi Ubungo, Dar es Salaam, unatajwa kwamba umakuwa ngome ya kurahisisha biashara hiyo kati ya China na Tanzania, ambako Watanzania wamekuwa wakisafiri kufuata bidhaa kuja kuziuza nchini.

Vilevile, kupitia ngome ya kivuli cha cha serikali madarakani, Shirika la Ndege la Tanzania (ATC), mbalo serikali inaifanyia maboresho mengo ya kimkakati, nayo ikatangaza kuanzisha safari za moja kwa moja kwenda China lengo ni kurahisisha biashara na kuwapa urahisi wafanyabiashara nchini, kwa kutumia nyenzo ya nyumbani kwao, hasa ikizingatiwa ATC sasa imenunua ndege kubwa ya kibiashara ya mizigo kukidhi mahitaji ya aina hiyo.

Inapoangaliwa katika mustakabali mpana, inapanua wigo wa kibiashara kati ya Tanzania na China, pia mataifa mengineyo yanayofika kuwekezaji nchini.

Hapo itakumbukwa, wawekezaji wa China wako nchini wamewekeza taifa sekta ya viwanda ambayo ni sehemu ya mkakati wa kiserikali tangu zama zilizopita hadi sasa katika awamu ya sita, kwenye wilaya kama ya Mkuranga mkoani Pwani kukiwapo ushuhuda huo.

Hiyo inaendana na hatua kubwa katika eneo la miundombinu, kwenye mabadiliko yenye kasi kubwa, sehemu kubwa ya kampuni za ujenzi mkubwa na haswa ya miradi ya Barabara, kandarasi zake ziko katika kampuni za Kichina zinazotajwa kumudu miradi mikubwa kwa ufanisi, huku ikiwa ni za gharama za chini.

Serikali hadi sasa imefanyia kazi nyendo hizo inayoungwa mkono na upande wa pili wa diplomasia uchumi, uhusiano wa kisiasa kati ya China na Tanzania ukidumu.

Tangu zama za awamu ya tano na zilizopita hadi sasa, kumeshuhudiwa uhusiano huo, baadhi moja kwa moja kisiasa chama tawala nchini China kikihusiana na nchini, katika ziara ambazo nyuma yake kunakuwapo timu kubwa ya wawekezaji kibiashara kiuchumi wanaoambatana nao kuanaglia fursa za kuwekeza nchini.

Vilevile, katika sura hiyo hivi karibuni kukashuhudiwa ziara ya Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, nchini China hali inayondeleza aina hiyo ya uhusiano tajwa, inayodhihirisha msimamo wa uongozi wa awamu iliyopo madarakani.

UCHUMI

KINACHOFANYIKA SHAMBANI VISIWANI...

# Wakulima wanavyopaa kwa mradi kilimo cha kisasa wasimamizi ni wanahabari kinamama

• Waliothubutu kwenye pasheni, wasimulia wanavyotabasamu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR



Mboga na matunda ya pesheni kutoka shambani, zikiuzwa jirani na shamba, Unguja. **PICHA: MTANDAO.**

ZANZIBAR ikiwa sasa inakabiliwa na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi kulikotokana na mambo mbalimbali, ikiwemo shughuli za kibinadamu visiwani humo, kunakopatikana Unguja na Pemba.

Kutokana na athari za mabadiliko hayo, sasa wakulima wanashauriwa kulima mazao yanayohimili mabadiliko ya hali ya hewa, ili kuzalisha mazao ya shamba, hata wakajiongezea kipato.

Miongoni mwa kilimo kinachohimili mabadiliko hayo ya hali ya hewa, kwenye zao la pasheni, tunda ambalo hutumika zaidi kwa matumizi ya juisi visiwani humo.

Baada ya wito na hitaji hilo la kiuchumi, sasa kuna wakulima Visiwani 'wameamka' na 'kufunguka masikio' wakisikia kwenye zao la matunda ya pasheni ambayo kwa sasa wanalima katika mfumo wa kilimo cha kisasa, kinachowaongezea mavuno, manufaa zaidi kushuhudiwa kwenye kipato,

Aviwa Songoro, mkulima wa kijiji cha Kizimbani Wilaya ya Magharibi 'A' Unguja, anasema ameachana na kilimo cha mboga baada ya kuona faida kubwa ya kilimo cha pasheni, ambayo soko lake ni zuri zaidi ikilinganishwa na mboga.

Mkulima huyo anasimulia kilichomshawishi kulima kilimo hicho, ni baada ya kupata elimu ya kilimo cha kisasa ya zao hilo, elimu ambayo amepata kupitia mradi wa viungo, mboga na matunda.

Ni mradi unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya na kutekelezwa katikia ubia wa miradi ya Community Forest Pemba (CFP), Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania - TAMWA ofisi ya Zanzibar, zikishirikiana na Wizara ya Kilimo ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mkulima Aviwa, anasema ni mwaka jana ndipo alipoanza kulima mboga, lakini soko lake lililkuwa dogo, hata kutokidhi mahitaji yake ya msingi, hadi sasa ameamua kujikita katika kilimo cha pasheni, akitaja kinambadilishia kwenye sura ya ufanisi.

"Soko la tunda hili la pasheni ni zuri sana, ukilinganisha na 'mbogamboga', maana kilo moja ya pasheni hufika hadi shilingi elfu tano, lakini pia kilimo hiki hakihitaji maji mengi na kinastahamili ukame," anasema mkulima Aviwa.

Pia, anasema mradi wa viungo ni mkombozi kwake umemtoa katika hali ngumu ya maisha na kwa sasa anapata kipato kinachomsaidia kuendesha familia ikiwamo kupata chakula na kusomesha watoto wake.

> **"Soko la tunda hili la pasheni ni zuri sana, ukilinganisha na 'mbogamboga', maana kilo moja ya pasheni hufika hadi shilingi elfu tano, lakini pia kilimo hiki hakihitaji maji mengi na kinastahamili ukame.**



Aviwa Songoro, akiwa katika shamba lake la mapasheni huko Kizimbani, nje ya Mji wa Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

Mkulima huyo anasema shamba lake lina ukubwa wa nusu ekari na kwa mavuno ya kwanza ya kilimo hicho alipata wastani wa fedha shilingi milioni moja na nusu baada ya kuvuna na kuuza.

Hata hivyo anasema, matarajio yake ni kuongeza uzalishaji wa zao hilo, ili kuendelea kupata kipato na kuondokana na ugumu wa Maisha, huku wakiajiri watu katika kilimo hicho.

Mkulima mwingine, Soud Mohamed Salum wa kijiji cha Kidimni wilayani humo, akiwa na hoja tangu kupata ujuzi wa kilimo kupitia mradi huo, sasa tija zaidi tofauti na alivyokuwa awali.

Anasema awali kilimo hicho wakulima wakilima kimazoea bila ya kujua faida yake na hivyo kukiona kama kilimo kisicho na faida.

Soud anasema, elimu aliyopatiwa kupitia mradi huo, imemsaidia kuongeza ubunifu na kuongeza uzalishaji mazao, ambayo kwa namna moja au nyingine, ni chachu ya kumuongezea kipato.

Anafafanua namna mradi huo umembadilisha maisha yake hasa kupitia kilimo cha zao pasheni, akiwa na uhakika wa soko akinufaika kwa asilimia kubwa anavuna kwa awamu tofauti, hali inayomsaidia kupata tija kwenye ustawi wa maisha yake.

Hapo, anatumia fursa hiyo akiwataka vijana kuacha kukaa mitaani na badala yake kujishirikisha katika kilimo, kwa sababu kitawasaidia kujikwamua na hali ngumu ya maisha.

### OFISA MRADI

Zulfa Bashiri Mbwana, ni Ofisa Masoko wa Mradi wa Viungo, anasema lengo lao ni kuongeza thamani ya bidhaa na kuhakikisha mnyororo wa thamani, unafikiwa kutoka kwa mkulima hadi mlaji.

Anasema kuna mafaniko makubwa kwa wanufaika wa mradi huo, ambao ni wakulima ikiwamo kuwatoa katika kilimo cha matumizi ya nyumbani na kulima kilimo cha biashara.

"Lengo kubwa tunayoitumia katika mradi bidhaa zetu zitengeneze historia,kwa mlaji na tunawashajihisha wakulima wetu kulima kilimo hai ambacho hakitumii kemikali,"anasema.

Pia, anataja inachangia hamasa kubwa, ikiwamo kuwa unganisha wakulima na masoko, hata kupata wanunuzi na mradi umelenga kuwasaidia wanufaika 21,000 na kwa sasa umeshaunganisha wanufaika kwa asilimia 60 kwa masoko ya ndani na nje.

"Kwa soko la nje tumejikita hasa katika mazao ya viungo, lakini kwa masoko ya ndani tuna mboga na mtunda hasa soko kuu lipo katika hoteli za kitalii,"anasema.

### MTAALAMU WA SEKTA

Shabani Peter, mtaalamu wa teknolojia ya uzalishaji na miundombinu ya wakulima kutoka mradi wa viungo, anasema lengo ni kuongeza uzalishaji kwa mkulima, katika kutimiza lengo ni kuhakikisha wakulima wanatumia teknolojia nzuri ya uzalishaji, inayoendana na mabadiliko ya hali ya hewa.

Peter, anasema kuhakikisha wakulima wanapata mbegu na miche bora, kuwa na mbinu bora za matumizi ya maji na kutoa elimu ya kutumia mbinu za matumizi sahihi ya maji.

Anasema, zaidi ya wakulima 100 wamewasadia miundombinu ya umwagiliaji maji wa mazao yao ili kuwa na matumizi sahihi ya maji na kutoa miche tofauti laki nane.

Mkulima huyo anasema, mradi huo umeboresha vitalu kwa wazalishaji katika jamii na sasa kuna vitalu vikuu vinne vinavyozalisha miche ikiwamo miche ya pasheni.

"Kwa sasa tunataka kutumia mbinu bora zaidi za umwagiliaji ambayo inatumia maji machache, kulingana na mabadiliko ya hali ya hewa kuna changamoto ya uhaba wa maji na ndio maana tunawahamasisha wakulima wetu kutumia mfumo wa umwagiliaji wa maji kidogo," anasema.

Sofia Ngalapi, Mkuu wa Mawasiliano wa Mradi wa Viungo kutoka TAMWA, anasema una lengo la kufungua fursa ya minyororo ya thamani kwa wakulima wadogo ambao wanalima mboga, matunda na viungo na lengo kuwafikia wanufaika zaidi ya 57,000 kwa Unguja na Pemba kwa kipindi cha miaka minne ambapo Juni mwakani, mradi huo utafikia kikomo.

Anawataka wakulima hasa wanawake pia kujikita katika kilimo cha bustani ya nyumbani ambao kilimo hicho, hakitumii eneo kubwa la ardhi na kinasaidia kupata lishe bora kwa familia na kuongeza kipato.

Mkurugenzi Mipango,Sera na Utafiti kutoka Wizara ya Kilimo, Maliasili na Umwagiliaji, Makame Kitwana Makame, anasema serikali ya Zanzibar, inawajali wananchi wake hasa wakulima wa viungo, mboga na matunda ili kujikwamua na hali ya maisha na kukuza kipato chao.


Mkurugenzi huyo anasema, serikali ni wasimamizi wakuu katika mradi huo wa viungo, kwa kuwapatia wakulima mafunzo na wataalamu ili wakulima kuendana na wakati uliyopo na kupata mazao mengi.

Aidha, anasema changamoto iliyojitokeza ni mabadiliko ya hali ya hewa na ukosefu wa soko kwa baadhi ya mazao, lakini serikali inaendelea kuifanyia kazi changamoto hizo, ili wakulima kupata soko la uhakika la kuuzia bidhaa zao wanazozalisha.

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Ama kweli DP World imejua kutuvuruga Watanzania!






**NA JOSEPH KULANGWA**
**(+255) 713 410008**
**kulangwasos@gmail.com**

ILIANZA kama utani vile! Jamani huku kuna mkataba Bunge linaomba watu wajitokeze kuutolea maoni kabla halijauridhia. Ni mkataba mzuri kuwahi kutokea katika nchi hii, unaolenga kuboresha bandari zetu na maisha yetu!

Ukiridhiwa huu na kuanza kutekelezwa, hakika nchi itakaribia pepo kwa kipato itakachokuwa kikiingia kupitia bandarini ambako miaka yote tumesimamia wenyewe lakini hasara tupu, bora sasa waje wawekezaji.

Bunge likaomba watu wajitokeze kwa siku moja tu kutoa maoni yao, ili mambo yasonge mbele. Watu wakataka kujua ni mkataba wa nani na nani au nini na nini au nani na nini? Jibu likaja kuwa ni serikali ya Tanzania na Dubai.

Ikafafanuliwa, kuwa kuna lijikampuni huko Dubai linaitwa Dubai Port World au DP World (DPW), lina mijitawi karibu duniani kote na linafanya kazi haijapata kutokea, likitumia mitambo ya kisasa na likija meli zitapakia na kupakuliwa kwa muda mfupi sana kuliko sasa.

Walioelewa watasema Mungu atupe gunia la chawa, ah wapi na tutoe maoni lijikampuni lije. Lakini maoni kwa siku moja itakuwaje sasa? Potelea pwete, katika nchi hii hakuna kinachoshindikana.

Ilikuwa tarehe sita mwezi wa sita. Yakafanyika. Juni 10 mwaka huu, Bunge likaidhinisha mkataba ukapita, na wale ambao hawakuwa wakijua nini kinaendelea, wakapata fursa ya kuusoma mkataba wenyewe. Duh wakashituka, mbona mambo yako segemnege hivi! Huu mkataba vipi?

Wakaibuka wanasiasa wa pande zote, watawala na wapinzani, maneno yakaibuka, nchi ikachangamka kwa majadiliano, wakaibuka wanasiasa wastaafu na wa sasa nao wakatazamana nyusoni, majasho yakiwachuruzika, wakiulizana nini hiki na kujibizana ndicho hicho unatakaje wewe? Lakini wote wanaunga mkono uwekezaji.

Wasiovumilia wakasukumiza mitusi, wakatukana na hata wasiotukanwa. Kwa mara ya kwanza nikaona heshima inashuka katika Taifa hili alilotuachia Nyerere Julius, vitoto vinatukana wazee bila kujali historia yao.

Wazee nao wanatukana vitoto bila kuangalia kuwa wanajishushia heshima zaidi, ili mradi vinywa vikajaa Dipiiwelidi kila kona.

Wanasiasa wengine wakaona hii si ndiyo kete, hasa wakati huu ikisalia miaka miwili ya uchaguzi wa serikali za mitaa na mkuu!

Wakajipanga kwa ziara mikoani kuhanikiza bandari zetu kuuzwa na serikali. Wa upande wa serikali na chama chao nao wakaona isiwe shida, nao wakapita mulemule walimopita wenzao kufukia mashimo, wakihanikiza hakuna bandari inauzwa.

Wanasheria huku, wataalamu kule, wanahabari huku wananchi wa kawaida kule, ilimradi ikawa songombingo, huku linasemwa hili kule lile, wa kuchanganyiwa hawakukosekana akijiaminisha kuwa ili mradi kula kupo lije lolote, kwani Dipiiwelidi ni mdudu gani mpaka liibue uzanzibari na utanganyika leo!

Wanasheria wengine wakaona kumaliza zahama hii ni kukimbilia mahakamani tu kuulizia kisheria kama lililofanywa na Bunge ni halali au haram kwani chuzi la mbwa bora linywewe lingali la moto.

Huku na kule, Mahakama ikasema kuna mambo madogo madogo, hayako sawa katika mkataba, lakini yanaweza kurekebishwa, lakini kubwa siye wakubwa hatuwezi kupinduliana meza. Bro akishaamua kaamua!

Waliokuwa wakitafuta ukweli kisheria wakatoka nje ya mahakama wakijiapiza kupanda ngazi ya juu ili kuutafuta ukweli zaidi kuhusu hilo, wakishangaa muhimili wa mahakama 'kuustahi' muhimili wa Bunge, wakisema ikishindikana hapo sasa ni sisi na kitaa tu!

Kilichotikisa sasa, ni pale walipojiapisha kuandamana bila kukoma kama mkataba usivyo na ukomo! Kumbe wameshika mkia wa nge.

Akaibuka bosi wa Polisi, homboi Wambura akawaambia thubutuuu. Niwaone kitaani eti mnaandamana. Ole wenu! Tena alichonishitua ni pale aliposema eti hawa jamaa wanataka kupindua Serikali ya Awamu ya Sita.

Nikajisemea moyoni si Tanzania hii ninayoijua miye. Tukitoka huko sasa tutachekwa na kila mtu, kwamba tunapindua nchi kwa sababu ya Dipiiwelidi kweli! Ahh Stupid!

Hivi Watanzania hebu tujiulize, kweli tumeamua kuitikisa nchi yetu hii yenye historia nzuri hivi, kwa kijikampuni tu cha kusimamia bandari kutoka Arabuni? Watu nje huko wanatufuatilia eti kwa sababu ya kiji-Dipiiwelidi kweli? Astaghafrulahi!

Ila tumejifunza, kwamba siku nyingine kama kuna vijimikataba kama hivi, basi wananchi tushirikishwe kikamilifu basi kuvijadili na kuona kama vinatufaa kwa wingi wetu au vinawafaa wao kwa uchache wao.

Haya yanayotokeatokea huko Afrika Magharibi tujue hayatokei hivihivi kwa kudra za Mwenyezi Mungu, ni kutokana na wenye nchi yao kutoridhishwa na mambo na hata kujikuta wamekuwa huko.

Kama tunahubiri demokrasia basi tuitekeleze na ionekane inatekelezwa.

**Alamsiki!**

BIASHARA

# Wakulima wa Korosho katika neema mpya wakibangua kwa mashine zao

**Na Christina Haule,** Morogoro

WAKULIMA wa zao la Korosho nchini wameanza kunufaika kwa kuwa na viwanda vidogo vya ubanguaji wa korosho na kuwaingizia kipato kinachosaidia kuondokana na umaskini, baada ya serikali kutilia mkazo mazao ya kimkakati.

Mmoja wa wakulima wa korosho, Flaviana Kiria mkazi wa Mzinga mkoani Morogoro, anasema akiwa mkulima wa mikorosho sita, anaona nafasi ya kupata mashine ya kubangua korosho ambayo ana imani ataitumia yeye pamoja na wakulima wenzake, huku akiwatoza malipo ya kubangua na kujiongezea kipato.

"Licha ya kwamba mashine itanisaidia katika kubangua korosho zangu chache, pia nitawalipisha na wenzangu wa maeneo ya jirani ambao wana mikorosho, lakini hawana mashine ya kubangulia, fedha ambayo itanisaidia kutatua changamoto zangu ndogo ndogo za kimaisha" anasema Kiria.

Anafafanua, baada ya kupata elimu juu ya ubora na faida ya kilimo hicho kwenye Maonyesho ya 30 ya Sikukuu ya Wakulima 'nanenane' Kanda ya Mashariki, ameamua kununua mashine hiyo ya kubangua korosho, sambamba na kuongeza ukubwa wa shamba lake ili akue zaidi kwenye kilimo cha biashara na kiuchumi.



Shughuli za kubangua korosho zikiendelea kiwandani. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



Ndivyo ilivyo mashine ya kubangua korosho kiwandani.

**BODI YA KOROSHO**

Kaimu Meneja wa Tawi Bodi ya Korosho mkoani Morogoro, Jafari Matata, anasema mkulima anayo nafasi ya kumiliki mashine ndogo ya kubangua korosho au kuanzisha kiwanda kidogo kwa kutumia mashine hiyo ambayo huuzwa kati ya shilingi 200, 000 hadi 300,000.

Matata anasema, kwa kuanzisha kiwanda kidogo anaweza kuwaruhusu wakulima wenzake kubangua korosho zao kwa gharama ya kuanzia shilingi1,000 kwa kilo moja na kujiongezea kipato.

Anasema zao la korosho lina masoko makubwa ndani na nje ya nchi na kwamba wakulima wana nafasi ya kulima kwa wingi na kuweza kuuza bila kuwa na wasiwasi kutokana na mpango wa kuuza korosho zilizobanguliwa na zilizoongezewa mnyororo wa thamani ambapo kilo moja ya korosho iliyoongezwa thamani huuzwa kwa Sh. 2400.

Hivyo, anawashawishi wakulima kubangua korosho wenyewe na kuziongeza thamani kabla ya kuziuza na hivyo kuona faida ya kilimo hicho.

Anasema mauzo ya korosho nje ya nchi huingiza fedha za kigeni nchini kwa kiasi kikubwa, tofauti na mazao mengine anataja zao linalofuata ni tumbaku.

Anazitaja nchi zinazonunua korosho kwa wingi Tanzania kuwa ni Pamoja na nchi za India na Vietnam.

Matata anasema, ni wakati umefika sasa kwa wakulima kutumia fursa hiyo katika kilimo sambamba na uwekezaji hasa kwenye ubanguaji wa korosho, akifafanua ni zao namba moja la kimkakati nchini na lina mapato makubwa, kwa sababu linalimwa katika mikoa mingi ya Tanzania.

Kwa sasa anataja mikoa ya Tanga, Pwani, Dodoma, Morogoro, Lindi, Mtwara, Iringa, Ruvuma, Singida, Tabora, Njombe, Katavi, Rukwa, Shinyanga, Tabora na Songwe. Matata anasema mkakati wa serikali mwaka 2025/26 ni Tanzania kuzalisha tani 700,000 za korosho kwa mwaka huo, huku ubanguaji ukilengwa ufike asilimia 60.

Anasema lengo la serikali sasa, ni kuhakikisha korosho zote za Tanzania ambazo ni tamu kupita zote duniani zinabanguliwa nchini ambayo huuzwa kwa kila tani moja ni sawa na Dola za Marekani, 160 ambayo ni sawa na shilingi laki 352,000.

> **Mwaka 2022 jumla ya miche 12,846,960 imegawiwa na mwaka 2021 miche 3,288,600 imegawiwa kwa wakulima wa korosho katika mikoa mbalimbali nchini.**

Hata hivyo, katika kukabiliana na elimu duni kwa wakulima juu ya magonjwa na upuliziaji wa dawa kwenye mikorosho shambani amewataka kuzingatia elimu wanazopewa mara kwa mara ili kuzalisha mazao bora yenye kuleta tija kwao na kwa taifa kwa ujumla.

Matata anasema, kila mwaka kwa kushirikiana na wasambazaji wa dawa hizo hutoa mafunzo kwa wakulima, serikali imetoa zaidi ya Sh. bilioni 130 kwa ajili ya kununua dawa za upuliziaji kwa msimu wa kilimo mwaka uliopita.

Hata hivyo, anasema toka mwaka 2016 hakukuwa na ruzuku ya ugawaji wa mbegu au miche ya mikorosho bure kwa wakulima lakini katika kuboresha kilimo na kuzingatia kilimo kwenye mazao ya kimkakati serikali kuanzia mwaka 2022 imeanza kugawa mbegu na miche bure kwa wakulima.

Anasema mwaka 2022 jumla ya miche 12,846,960 imegawiwa na mwaka 2021 miche 3,288,600 imegawiwa kwa wakulima wa korosho katika mikoa mbalimbali nchini.

Mkurugenzi wa Kilimo na ubanguaji kutoka Bosi ya Korosho Tanzania, Luseshelo Silomba, anasema serikali imeendelea kuongeza ubanguaji wa korosho hapa nchini ikiwa ni pamoja na kuruhusu uwepo wa soko la awali na kuhamasisha uwekezaji kwenye ubanguaji.

Anasema katika msimu huu kuna viwanda vipya sita vimefunguliwa vyenye uwezo wa kubangua tani 28,600 za korosho,hivyo kuongeza uwezo wa viwanda vya kubangua hadi kufikia tani 64,000 za korosho ghafi.

Anataja hivi karibuni wamefungua soko la Marekani la kuuza korosho zilizobanguliwa na kufungashwa katika vikasha na vifungashio kwa ajili ya mlaji na kwamba upanuzi wa soko hilo utachagiza uuzaji wa korosho iliyobanguliwa kutoka Tanzania.

Pia, anasema kumekuwa na ongezeko la uzalishaji wa mafuta ya ganda ya korosho, ambazo katika msimu uliopita, jumla ya lita 55,000 ziliuzwa nje ya nchi.

Anasema Bodi ya Korosho Tanzania ina mpango wa kujenga kiwanda cha mfano kitakachotumika kwa ajili ya mafunzo na kumalizia uchakataji wa korosho iliyobanguliwa kutoka katika viwanda vingine ambavyo havikidhi viwango ikiwa ni pamoja na korosho kutoka katika vikundi vya ubanguaji na wabanguaji mmoja mmoja.





Spika mstaafu na Mbunge wa Kongwa, Job Ndugai (kulia), akisalimiana na Mwenyekiti wa kijiji cha Mkoka, Elia Chibago baada ya kuwasili kwa ajili ya shughuli za maendeleo jimboni kwake Wilaya ya Kongwa Mkoani Dodoma jana **PICHA: IBRAHIM JOSEPH.**

# RC afichua siri walimu kushindwa kufundisha

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, amesema walimu wanakopa mikopo mingi katika taasisi za fedha na watu binafsi hali inayowasababishia wasizingatie kufundisha.

Amesema pia baadhi ya maofisa utumishi wanapewa rushwa ili wasaini kuridhia walimu kupewa mikopo hiyo.

Aliyasema hayo jana kwenye kikao cha wadau wa elimu kilichoandaliwa na Chama cha Walimu Tanzania (CWT) Mkoa wa Singida kwa lengo la kupanga mikakati ya namna ya kukabiliana na kero zilizopo katika mkoa wake ikiwamo kufanya vibaya katika matokeo ya mitihani ya taifa ya darasa la saba, kidato cha pili na cha nne.

Alisema kutokana na walimu hao kukopeshwa mikopo mingi wanajikuta mishahara yao inaishia kulipa madeni na hivyo wanashindwa kufundisha vizuri wanafunzi darasani kutokana na kuwa na mawazo kwa sababu wanakuwa hawana kitu mifukoni.

"Maofisa utumishi mnasaini wale makanjanja wanakuja kwenu wanakwambia saini kuna mwalimu fulani nataka nimkopeshe na hujali kama amemaliza mikopo mingine aliyokopa na makanjanja hawa wengine wanakuja wanawapa rushwa ili msaini na matokeo yake mshahara wa mwalimu unaishia kulipa madeni, mwalimu huyu hawezi kufanya kazi kwa bidii," alisema.

Alisema sheria inaeleza kwamba mtumishi asikope zaidi inatakiwa abakiwe na theluthi moja ya mshahara wake, lakini maofisa utumishi wanaruhusu walimu wakopeshwe mikopo mingi kwenye benki, taasisi za fedha na kwa watu binafsi jambo ambalo halikubaliki.

Kufuatia hali hiyo, Serukamba aliwaagiza wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya na maofisa utumishi kuitisha mikutano na walimu kuwaeleza kwamba hairuhusiwi kukopa zaidi. "Tuwe wakali tusikubali walimu wakope zaidi ya kile wanachostahili kukopa na tuwaelimishe wakope kwenye taasisi zinazoeleweka ambazo riba sio kubwa," alisema.

Kadhalika, alitaja sababu nyingine za walimu kutokuwa na ari ya kufundisha vizuri ni lugha mbaya inayotolewa na baadhi ya maafisa elimu na wengine dhidi ya walimu, kutopandishwa madaraja kwa wakati na kutolipwa stahiki zao kwa wakati.

Naye, Katibu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) Mkoa wa Singida, Digna Nyaki, alisema kumekuwa na changamoto walimu wanapostaafu wakurugenzi hawawalipi hela ya mizigo kwa ajili ya kurudi kwao.

Nyaki aliipongeza serikali kwa hatua mbalimbali zinazochukuliwa na serikali katika kuboresha maslahi ya watumishi wakiwamo walimu na kuwapandisha madaraja.

# Wakulima wapewa mbinu ya kujiinua kiuchumi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAKULIMA wametakiwa kutumia fursa ya mkutano wa kujadili mifumo ya chakula Afrika, kwa ajili ya kutafuta masoko ya mazao mbalimbali ili kujiinua kiuchumi, kujitangaza kimataifa kwenye sekta ya kilimo.

Mkutano huo umepangwa kufanyika Septemba tano hadi Nane katika ukumbi wa mikutano wa kimataifa JNICC, uliopo mkoani Dar es Salaam.

Akizungumza jana jijini hapa Mkurugenzi wa Mpango wa Kuendeleza Kilimo Ukanda wa Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania- (SAGCOT), Geoffrey Kirenga alisema kuwa mkutano huo ni fursa za kipekee kwa wakulima kujipatia masoko ya kuuza mazao yao ya kilimo kwenda nje ya nchi.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan amewakaribisha wadau wa kilimo pamoja na wananchi kwa ujumla kujiandikisha kwa ajili ya kushiriki kwenye mkutano huo hivyo nao wanapaswa kutumia fursa hiyo kujitangaza kwenye sekta ya kilimo. "Serikali imekaribisha viongozi wengi kutoka ndani na nje ya nchi, hivyo wakulima nao wajitokeze kwa wingi ili kushiriki mkutano huo ambao ni muhimu kwa wakulima,"alisema Kirenga.

Alifafanua zaidi ya kuwa mkutano huo utajumuisha wakuu wa nchi kadhaa kutoka ndani na nje ya Afrika, wakuu wa mashirika ya kimataifa, wawekezaji, mawaziri pamoja na wadau wengine wakubwa wa kimataifa wapatao 3,000.

Alisema pamoja na mambo mengine kutakuwa na fursa za uwekezaji kutoka kwa wadau wa kilimo wa ndani ya nchi kuwakaribisha wawekezaji wa nje kwenye miradi yao, ikiwemo kubadilishana fursa za kibiashara na mazao.

Mkurugenzi huyo alisema katika hamasa ya kukaribisha wageni nchini kushiriki katika mkutano huo, Rais Samia amekuwa mfano wa kuigwa kwa kuzidi kuiweka Tanzania katika ramani moja nchi zenye kuzidi kukuza sekta ya kilimo.

Alisema katika sekta ya kilimo serikali imeweka jitihada ya kuhamasisha vijana na wanawake katika kilimo biashara ikiwemo kuwapa fursa mbalimbali za kujiinua kiuchumi kupitia biashara. Kirenga alisema kuwa SAGCOT ikiwa kama mwavuli wa kampuni nyingi za kilimo pamoja na vyama vya wakulima na mkulima, ipo tayari kushirikiana na serikali katika kuhakikisha kuwa kila fursa inayotakiwa kumnufaisha mkulima kupitia jukwaa hilo inamfikia mkulima husika.

Alisema wana kila sababu ya kuwahimiza wakulima na wafanyabiashara kushiriki katika mkutano huo ili waweze kujitangaza kimataifa, ikiwemo kuingia kwenye soko la ushindani.

# Viongozi taasisi za umma wataja faida kubadilishana taarifa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

VIONGOZI kutoka taasisi za umma wameeleza faida za kubadilishana taarifa kidijitali kupitia Mfumo wa pamoja wa Ubadilishanaji Taarifa Serikalini (GovESB) ikiwamo kupunguza gharama za uendeshaji.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, viongozi hao walieleza kuwa mfumo wa GoVESB umekuwa na faida nyingi ikiwemo kuongeza ufanisi wa utendaji kazi, kuokoa muda pamoja na gharama za uendeshaji wa taasisi.

Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Prof. Elisante Ole Gabriel, alisema Mahakama inabadilishana taarifa na taasisi mbalimbali ikiwemo Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

"Mfumo wa GoVESB umesaidia kuongeza ufanisi katika utendaji kazi wa Mahakama kwa kuwa tunaweza kupata taarifa kwa urahisi kutoka taasisi tulizoingia nazo makubaliano na kuweza kubadilishana taarifa kidijitali, vilevile umesaidia kuongeza ufanisi na uwazi katika kuwahudumia wananchi kwa wakati", alisema Prof. Elisante.

Naye, Mkurugenzi wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), Herman Mandari, alisema kabla ya kuanza kutumia mfumo wa GovESB, chuo hicho kilikuwa kikikabiliwa na tatizo la upatikanaji wa taarifa kutoka taasisi mbalimbali za umma.

"Kabla ya kuanza kutumia mfumo wa GoVESB, maofisa walilazimika kuwasilisha maombi ya kupata taarifa kwa njia ya barua kwa kutembelea taasisi husika, hivyo kuchukua muda mrefu kupata taarifa hizo, jambo lilichongia kupunguza ufanisi katika utendaji wa kazi", alisema Mandari.

Kaimu Meneja wa TEHAMA Chuo cha Utumishi wa Umma, Elibariki Mushi, alisema mfumo wa GovESB umewasaidia kupata taarifa sahihi zinazoaminika na zenye ubora na viwango stahiki kwa wakati, hivyo kuimarika kwa usalama wa upatikanaji wa taarifa.

"Taarifa hizi tunazipata sehemu moja, hili ni jambo jema na mwelekeo huu ndiyo ulikuwa unasisitizwa na viongozi wetu, hivyo sio tu tunabadilishana taarifa ila tutabadilishana taarifa katika viwango vinavyofanana,"alisema Mushi.

Kaimu Mkuu wa Chuo cha Biashara (CBE), Prof. Edda Lwoga, alitoa hamasa kwa taasisi za umma ambazo hazijajiunga na mfumo wa GovESB kujiunga na mfumo huo.

Aidha, Katibu Mtendaji Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET), Dk. Adolf Rutayuga, alizishauri taasisi za umma kujiunga katika mfumo huo ili kuokoa muda wa kuwahudumia wananchi, lakini pia kupunguza gharama za kutengeneza mifumo midogo midogo ya kuunganisha na taasisi nyingine.

Mfumo wa GoVESB umetengenezwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa kuzingatia Kifungu cha 48 (2) cha Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya Mwaka 2019, kinachoitaka Mamlaka ya Serikali Mtandao kuanzisha na kuendesha mfumo unaowezesha mifumo ya TEHAMA serikalini kuwasiliana na kubadilishana taarifa.






Mwenyekiti kikundi cha uvumilivu kupitia shirika mama la Island of Peace (IDP), Bakari Sumawe (kulia), akitoa maelezo kwa watu waliotembelea meza yake kuhusu mbegu mbalimbali wakati wa mkutano wa kimataifa wa wadau wa mbegu asili kuhusu kuona namna ya kuzilinda, kuzitunza na kuziendeleza, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# TUGHE yataja mwarobaini mikopo umiza kwa wafanyakazi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

CHAMA cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya (TUGHE) mkoani Njombe, kimesema mwarobaini wa mikopo umiza kwa wafanyakazi ni kuunda Saccos kuanzia ngazi za matawi ili kuwasaidia wanachama.

Mkakati huo ulielezwa na Mwenyekiti wa chama hicho, Mkoa wa Njombe, Dk. Mashaka Kisulila wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema chama hicho kimeenda mbali zaidi kwa kuhakikisha wafanyakazi wanakuwa na kipato, wanajiepusha na mikopo umiza kwa kuanzisha mfumo wa kukopesha wafanyakazi kutokana na fedha za asilimia mbili ambazo huchangiwa na wanachama.

"Kwenye hospitali yetu ya mkoa kuna taasisi ya kukopeshana Saccos kwa hiyo maana yake itapunguza ukali wa maisha na mwanachama tunampunguzia kasi ya kwenda kujiingiza kwenye mikopo umiza ya mitaani"alisema Dk. Kisulila.

Dk. Kisulila aliwataka wafanyakazi kujiunga na vyama vya wafanyakazi ili kuwa na sauti ya pamoja katika kupigania haki kazini, maslahi na mikataba rafiki.

Aidha, alisema bado kuna changamoto ya baadhi ya wafanyakazi kuwa na mwamko mdogo wa kujiunga na vyama vya wafanyakazi licha ya faida zilizopo. Baadhi ya wanachama wa TUGHE akiwemo, Harison Serenga alisema mikopo hiyo inawanufaisha kwa sababu mshahara pekee hauwezi kukidhi mahitaji ya mfanyakazi.

Alisema: "Napata manufaa kwa sababu hizi fedha tunakopeshana alafu riba yake inakuwa ni ndogo sana ni tofauti na taasisi nyingine ambazo tumekuwa tukikopa kwa riba kubwa".

# 'Wafugaji tumieni maabara ya veterinari kuepuka hasara'

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA.

WAFUGAJI nchini wametakiwa kuitumia Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) ili kuleta ufanisi kwenye uzalishaji kupitia sekta hiyo na kuepukana na hasara itokanayo na changamoto mbalimbali ikiwemo maradhi ya mifugo.

Kwa mujibu wa Mtendaji Mkuu TVLA, Dk. Stella Bitanyi tayari wakala hiyo ina jumla ya vituo 13 nchini vinavyoendelea kutoa huduma kwa wananchi hususani wadau wa sekta ya mifugo.

Dk. Bitanyi alibainisha hayo alipozungumza na Nipashe na kusema kuwa miongoni mwa majukumu iliyopewa TVLA iliyo chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni pamoja na kufanya uchunguzi na utambuzi wa magonjwa ya mifugo kupitia vituo vyake.

Alisema majukumu mengine ni kuzalisha chanjo za mifugo pamoja na utafiti, kufanya udhibiti wa ubora wa vyakula vya mifugo kwa maana ya kujua ubora kwa kuvipima na kutoa ushauri.

Nyingine ni kupima ubora na kusajiri viuatililu vya mifugo pamoja na kutoa mafunzo kwa wahitimu wa ngazi mbalimbali za elimu inayohusu ufugaji.

"Upimaji ubora wa viuatilifu vya mifugo na vilevile kusajiri ni jukumu jipya tumelianza toka Septemba mwaka jana. Awali jukumu hili lilikuwa linafanywa na TPRI kule Arusha lakini sasa hivi limerudi Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa sababu ni viuatilifu vya wanyama na wakala tumepewa jukumu hilo." Alifafanua Dk Bitanyi.

Alisema kwa upande wa mafunzo wanatoka katika ngazi mbalimbali ikiwemo kwa wanafunzi wa kuanzia stashahada, shahada na elimu za juu zaidi na pia kwa wananchi ambao ni wafugaji kwa kushirikiana na maofisa mifugo waliopo kwenye halmashauri mbalimbali nchini. Alisema kwa sasa wanawafikia wafugaji kwa kiwango kikubwa kupitia vituo vyao ambavyo wataalamu huwatembelea wafugaji kwenye maeneo yao hususani wilayani na vijijini.

Alisema pia wana programu mbalimbali za kutoka kwenda kutoa mafunzo kwenye mashamba.

Alisema kupitia kuwafikia wakulima ndipo wakala hiyo inapata uwezo wa kuchukua sampuli za magonjwa ya wanyama au mimea ya vyakula vya mifugo na kujua hali iliyopo kwa ajili ya kuleta tija kwa wafugaji.

Aidha, Dk. Bitanyi alisema pia wamekuwa wakitumia maonesho mbalimbali yakiwemo ya Nanenane kama walivyofanya kwenye vituo mbalimbali mwaka huu ikiwemo kwenye Uwanja wa John Mwakangale mkoani Mbeya yalikofanyika kitaifa na pia kwenye kanda nyingine yalikofanyika.

Alisema kwa maonyesho ya Nanenane mwaka huu wafugaji wengi waliojitokeza kwenye mabanda ya TVLA ni walio na changamoto za kushindwa kudhibiti magonjwa ya mifugo hasa kwa ng'ombe na kuku hatua inayowasababishia kuwa na uzalishaji hafifu.

Kwa mujibu wa Dk. Vitanyi, vituo 13 vya TVLA vipo Sumbawanga mkoani Rukwa, Kigoma, Tabora, Meatu mkoani Simiyu, Mwanza, Arusha, Tanga, Dodoma, Iringa, Mtwara, Kibaha mkoani Pwani palipo na Kiwanda cha Chanjo na Dar es Salaam ambayo ni makao makuu ya wakala.

# Watanzania waitwa kuwekeza miundombinu kwenye utalii

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

WAWEKEZAJI wazawa wamealikwa kuwekeza miundombinu kwenye vivutio vya utalii vilivyopo wilayani Rungwe ili kunufaika na fursa ya watalii wanaofika kwa wingi.

Ofisa Utalii wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Anumwagile Bugali alibainisha hayo wakati akizungumza na Nipashe ambapo alisema jumla ya vivutio 25 vimeainishwa wilayani hapa ikiwamo Hifadhi ya Mlima Rungwe, Ziwa Ngosi Daraja la Mungu pamoja na Kijungu.

Bugali alivitaja vivutio vingine kuwa ni maporomoko 16 ya maji yaliyopo wilayani hapa yakiwemo ya Kaporogwe, Isabula, Malasusa na Kapiki.

"Tunacho kivutio cha mti katembo pia. Unaitwa jina hilo kutokana na ukubwa wake. Wenyeji wamewapa jina hilo kwa sababu ni mti ambao watu wazima wasiopungua 12 ndiyo wanaweza kuuzunguka kwa kushikana mikono. Lakini pia yapo majengo ya kale yaliyo na historia na simulizi mbalimbali." alisema Bugali.

Ofisa Utalii huyo alisema katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, imeweka jitihada mbalimbali juu ya namna ya kuboresha vivutio hivyo na kuvitangaza.

Alisema kwa kushirikiana na wadau mbalimbali tayari uwekezaji wa miundombinu umefanyika kwenye baadhi ya vivutio hususani cha Ziwa Kisiba ambacho sasa kinatembelewa zaidi na watalii kutokana na miundombinu kuboreshwa na upatikanaji wa huduma muhimu.

Alisema pia Ziwa Ngosi tayari limekuwa na miundombinu kwa maana ya kuwepo kwa barabara na huduma mbalimbali anazoweza kuzipata mtalii anapotembelea ikiwemo kambi za kupumzika, vyoo na nyinginezo. Alisema pamoja na uwekezaji huo bado vipo vivutio vingine vinavyohitaji wawekezaji zaidi kutokana na utalii kukua hasa baada ya Filamu ya Royal Tour ambao pia utalii wa ndani umekuwa.

"Kwa sasa takwimu zinaonesha kwa halmashauri yetu watalii wanaotembelea zaidi vivutio vyetu ni wa ndani. Hii inaonesha baada ya Filamu ya The Royal Tour kila mtanzania amehamasika kutembelea vivutio vilivyopo. Kumekuwa na uelewa mkubwa kuwa utalii siyo wa wazungu pekee bali hata Watanzania wanauweza," alisema.

Alizitaja fursa za uwekezaji zilizopo kwenye vivutio kuwa ni pamoja na ujenzi wa hoteli, migahawa, uundaji vikundi vya ngoma za asili, upikaji vyakula vya asili na ujenzi wa kambi za kupumzika kwakuwa watalii wanaovitembelea wanahitaji kupata huduma mbalimbali.





# Dk. Mwinyi: Maji ni ufunguo wa maendeleo sekta mbalimbali

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema maendeleo ya sekta ya afya, elimu, kilimo, ufugaji, viwanda, miundombinu, utalii na uwekezaji yanahitaji uwepo wa huduma za maji ya uhakika.

Aliyasema hayo wakati akifungua kongamano la maji Zanzibar na kueleza kuwa lazima kuwe na mipango imara na thabiti ya utafiti zinazohusiana na maji.

Alisema tafiti hizo zitasaidia kupata ufumbuzi wa tatizo la upatikanaji wa maji ili kuongeza kasi katika kuendeleza sekta hiyo.

Dk. Mwinyi alisema dunia inakabiliwa na ongezeko la idadi ya watu, mabadiliko ya tabianchi na kushuhudia changamoto kubwa ya upungufu wa maji baada ya vyanzo vikuu vya maji kuathirika kutokana na majanga hayo.

"Tafiti mbalimbali zimethibitisha kwamba mabadiliko ya tabianchi na ongezeko la idadi ya watu yamekuwa yakisababisha kupungua kwa uzalishaji wa huduma ya maji katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara" alisema.

Dk. Mwinyi aliitaka jamii kuendelea kuimarisha mazingira kwa kupanda miti ambayo ni muhimu kwa upatikanaji wa mvua, kuendelea kuilinda miundombinu ya maji na kuvilinda vyanzo vya maji vilivyopo kwa kuviepusha na shughuli zao zikiwemo za ujenzi na makazi.

Aidha, alisema zipo tafiti zilizofanywa na kuonesha kuwa zaidi ya watu milioni 748 hawana maji safi na salama duniani kote.

Dk. Mwinyi alisema takwimu zilizopo zinaonesha zaidi ya watu milioni nne wanafariki kila mwaka kutokana na ukosefu wa maji kunakosababishwa na mambo kadhaa yakiwamo uchafuzi wa mazingira kunakosababishwa na viwanda, mabadiliko ya hali ya hewa na kuwepo kwa miundombinu chakavu.

Hata hivyo, alisema Zanzibar inategemea zaidi maji yaliopo chini ya ardhi kwa uchimbaji wa visima au kutoka kwenye chemchem ziliopo.

Dk. Mwinyi alisema Zanzibar bado haijaweza kuwa na mitambo na nyenzo za kutosha kwa ajili ya kuyageuza maji ya chumvi kuwa maji baridi kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

"Kwa msingi huo, kwa miaka ijayo bado tutaendelea kutegemea maji yaliyoko chini ya ardhi kuwa ndio chanzo chetu kikuu cha maji safi na salama.

Kwa hivyo, natumia fursa hii kusisitiza kwamba usimamizi endelevu wa rasilimali maji chini ya ardhi, kwetu sisi ni suala la lazima hasa katika wakati huu ambapo athari za mabadiliko ya tabianchi zinazidi kuongezeka"alisema.

Alisema serikali itaendelea kufanya tafiti zitakazoonyesha njia bora zaidi ya uvunaji wa maji ya mvua katika mabwawa, ili kutafuta vyanzo vyingine vya maji na hatimaye kuongeza ufanisi katika sekta hiyo kwa manufaa ya wananchi.

Dk Mwinyi aliwataka viongozi wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini, kuhakikisha wanafanya kazi kwa karibu na watafiti wanaofanya utafiti katika sekta ya maji ili kuwe na mpango madhubuti wa kukusanya na kutumia matokeo ya tafiti zinazofanywa Zanzibar kwa maendeleo ya nchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Global Water Partnership Tanzania, Dk. Victor Kongo akizungumzia kongamano hilo alisema taasisi yake itaendelea kushirikiana na Zanzibar katika kuhakikisha tatizo la maji linaondoka.

Waziri wa Maji, Nishati na Madini, Shaibu Hassan Kaduara, alieleza nia ya Serikali ya Zanzibar katika jitihada za kuwafikishia wananchi huduma za maji safi na salama.

Alisema Septemba mwaka huu serikali kwa mara ya kwanza inatarajia kuzindua tangi la maji la lita milioni 32, ambalo litasambaza maji kwenye maeneo mengi ya Zanzibar.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi akipata maelezo kutoka kwa Meneja wa Usambazaji maji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Mhandisi Tyson Mkindi alipotembelea banda la DAWASA kwenye kongamano la utekelezaji wa programu ya uwekezaji kwenye sekta ya Maji, linaoendelea jijini Zanzibar. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wizara yapewa jukumu kuweka ubora vituo vya afya

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar imetakiwa kuhakikisha kwamba ujenzi wa vituo vya afya ya msingi vinakuwa na sifa ya kuwepo kwa huduma za kinamama na watoto kwa ajili ya kudhibiti vifo vinavyotokana na uzazi.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Viongozi wakuu wa Kitaifa wa Baraza la Wawakilishi, Mtumwa Peya Yussuf, aliyasema hayo wakati alipofanya ziara kukagua vituo vya afya ya msingi ikiwamo cha Bumbwini Wilaya ya Kaskazini B Unguja.

Alisema vituo vya afya ya msingi vilivyopo vijijini ndiyo tegemeo la wananchi wengi kupata huduma za afya na matibabu katika hatua ya awali wakati wanapokabiliwa na maradhi mbalimbali.

Alisema vifo vya kinamama na watoto vitapunguwa endapo juhudi za kuimarisha vituo hivyo zitachukuliwa na uongozi wa Wizara ya Afya.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dk. Fatuma Mrisho alisema wamejipanga kujenga zaidi ya vituo vya afya ya msingi 150 Unguja na Pemba ikiwa ni sehemu ya mikakati ya kutoa huduma za afya katika hatua ya awali kukabiliana na maradhi.

Alisema ujenzi wa Kituo cha Afya cha Bumbwini ni sehemu ya mikakati hiyo kuona huduma hizo zinawafikia wananchi wote, kwamba mkazo umewekwa katika kudhibiti vifo vinavyotokana na kinamama.

Aidha, alisema takwimu za vifo vya kinamama na watoto zinaonesha kupungua ambapo vifo vya Watoto vimeshuka kutoka 542 mwaka 2021 hadi 421 mwaka 2022.

Alisema wakati umefika kwa familia pamoja na kinamama kuzingatia uzazi wa mpangilio ambao unaonekana ni miongoni mwa njia za kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi, Mwantatu Mbaraka Khamis, alisema kukamilika kwa hospitali 11 za wilaya ni miongoni mwa hatua za kukabiliana na kupunguza vifo vinavyotokana uzazi.

# TFCG yamaliza mgogoro wa ardhi uliodumu miaka 10

**Na Rahma Suleiman, aliyekuwa**
MUHEZA

SHIRIKA la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) kupitia mradi wa kuunganisha misitu ya asili ya Amani na Nilo, umefanikiwa kutatua mgogoro wa ardhi uliodumu kwa miaka 10 kati ya Kijiji cha Kwezitu na Antakae wilayani Muheza mkoani Tanga.

Vijiji hivyo ni miongoni mwa vijiji saba vilivyozungukwa na ushoroba wa Msitu wa Asili wa Hifadhi ya Amani- Nilo ambavyo vilikuwa na mgogoro wa mipaka ya ardhi.

Mradi huo wa kuunganisha misitu ya asili ya Amani na Nilo unaotekelezwa katika vijiji saba ambavyo ni Kizerui, Antakae, Msasa IBC, Migoda, Shembangeda, Kwezitu na Kwemdimu, kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS).

Wengine ni sekta binafsi, wakulima wadogo na jamii inayozunguka eneo la mradi na kufadhiliwa na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Watu wa Marekani (USAID) chini ya Mradi wa Tuhifadhi Maliasi.

Akizungumza na waandishi wa habari wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET) wilayani Muheza mkoani Tanga, ofisa anaeshughulikia mipango bora ya ardhi kutoka TFCG, Ewald Gervas Emil, alisema suala la ardhi ni changamoto kubwa kwa sababu maeneo mengi yamo katika hifadhi ya msitu na ndiyo sababu migogoro ya ardhi inajitokeza.

Alisema rasilimali ardhi haiongezeki lakini binadamu wanaongezeka, hivyo kusababisha mahitaji ya ardhi kuongezeka kila siku.

Alisema ongezeko hilo limesababisha changamoto nyingi katika maeneo mengi ya vijiji hivyo, ikiwemo matumizi yasiyo endelevu ya rasilimali za misitu na migogoro ya ardhi.

Kadhalika, alisema kwenye eneo la ushoroba kuna misitu midogo ambayo imo katika ardhi za vijiji na kwa bahati mbaya maeneo hayo yameathirika na shughuli za kiuchumi hasa kilimo.

Alisema shughuli za kibinadamu katika ushoroba zikiathiri muunganiko wa misitu ya mazingira asilia ya Nilo na Amani, hivyo TFG huviwezesha vijiji hivyo kuwa na matumizi bora ya ardhi.

Alisema uharibifu wa mazingira ni mkubwa kutokana na mahitaji ya ardhi kwa shughuli za kilimo na zingine, hivyo ni vyema vijiji vilivyozungukwa na msitu huo kuwawezesha kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi.

Alisema mradi huo una lengo la kuazisha shughuli za kuongeza kipato kwa wananchi wa vijiji hivyo ili kuacha kuharibu misitu.

Mkuregenzi wa JET, John Chikomo, alisema iwapo wadau wa mazingira na uhifadhi watawawezesha wananchi wa vijiji vilivyozunguka hifadhi ya misitu kuwa na vyanzo vingine vya mapato wataachana na uharibifu wa misitu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA RUFANI YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**SHAURI LA RUFAA YA MADAI NA.27 LA MWAKA 2021**
**GLORIA IRIRA.......MRUFANI**
**DHIDI YA**
**SUDI MRISHO NGWAMBI.......MRUFANIWA NA. 1**
**MUJITABA KURBAN SELEMWALLA...MRUFANIWA NA. 2**
**ASHOK BHAILAL SHANGHAVI......MRUFANIWA NA. 3**

**KWA:**
**ASHOK BHAILAL SHANGHAVI**

**POPOTE ULIPO**

Unajulishwa kwamba shauri la Rufaa ya madai tajwa hapo juu limepangwa kusikilizwa na Mahakama hii hapa Dar es Salaam tarehe 29/08/2023 saa tatu kamili asubuhi (9:00).
Unapaswa kuhudhuria siku na tarehe iliyopangwa bila kukosa na endapo hutahudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi wako anayetambulika kisheria rufaa itasikilizwa bila ya uwepo wako.
Imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 16/08/2023.

J. E. FOVO
Kny: MSAJILI
MAHAKAMA YA RUFANI

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.96 of 2023**
**In the matter of the Estate of the late YUSUFU ALFONCO MKOMWA of Viwandani within Dodoma city**
**And**
**In the matter of Application for letters of Administration by JOHN KIONDO MDACHI**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules GN 369 of 1963)**

All persons claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 31 day of 8, 2023
Dated at Dodoma this 11 day of August 2023

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE DODOMA DISTRICT

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

JOSHUA ELIMSU MAKUNDI anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili T 400 CEX aina ya Toyota NADIA Chassis No. SXN150008425, Engine No.3S0236541. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu.
Taarifa ya polisi; DOD/DOD/RB/270039/2023

---

## KUPOTEA KWA OFA YA KIWANJA

**CHRISTINA PAUL**

anatangaza kupotelewa na ofa ya kiwanja PLT NO. 25 BLOCK F – IPAGALA NORTH – Dodoma City Council. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu.
Taarifa ya Polisi:
**DOD/DOD/RB/259009/2023**

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA TEMEKE**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI 235 YA 2019 & 33/2020**
**Nyanza Cooperative Union (1984) LTD......MDAI/WADAI**
**DHIDI YA**
**Abdul Quabid Ally Abdallah......MDAIWA/WADAIWA**

### KUITWA SHAURINI

Abdul Quabid Ally Abdallah POPOTE ULIPO/MLIPO Nyanza Cooperative Union (1984) Ltd. Amefungua/wamefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba Temeke. Shauri husika limepangwa HUKUMU TAREHE 21/08/2023 saa 3:00 Asubuhi Mbele ya Mh. L. R. Rugarabamu Mwenyekiti wa Baraza.
Unatakiwa ufike/mfike wewe/nyinyi/au wakili wako/wenu mwakilishi wako/wenu pasipo kukosa.
AMRI hii imetolewa na kutiwa Saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 16 mwezi 08 mwaka 2023.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA TEMEKE

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA BABATI**
**LILILOPO BABATI**
**MAOMBI NA 25 YA 2023**
**EMANUEL PAULO............................ MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**1.DANIEL BURA............................WAJIBU MAOMBI**
**2.MUSSA GABRIEL**

**Mdaiwa popote ulipo(DANIEL BURA).**
Fahamu kwamba mleta Maombi(Emanuel Paulo) ameleta Maombi Na. 25/2023 dhidi yako.
Hivyo basi kama unakusudia kupinga Maombi hayo unatakiwa kuleta majibu yako na uwepo Barazani wewe binafsi, wakili wako au mwakilishi anayetambulika kisheria, Shauri limepangwa kutajwa tarehe 5/9/2023.
Endapo hautatekeleza hiyo shauri litasikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa maamuzi.
Imetolewa na kutiwa Saini na mhuri wa Baraza hili leo tarehe 15/8/2023.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) BABATI

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA DODOMA**
**MAPITIO YA MADAI NA. 3/2023**
**HASSAN MOHAMED ........................MWOMBAJI**
**NA**
**ANTONIO ZANETTI...........................MJIBU MAOMBI**
**KWA:**
**ANTONIO ZANETTI**
**POPOTE PALE ULIPO**
**YAH: TAARIFA YA KUSIKILIZWA KWA MAPITIO YA MADAI NA. 3/2023**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DODOMA**
UNAFAHAMISHWA KWAMBA: Shauri tajwa hapo juu litasikilizwa Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda Dodoma, Mbele ya Jaji, S. H. Hassan, wa Mahakama Kuu Dodoma, saa tatu (3:00) asubuhi siku ya Jumatatu tarehe 02/10/2023.
HIVYO BASI; unatakiwa ufike wewe mwenyewe au Wakili wako siku hiyo iliyotajwa bila kukosa.
NA ENDAPO; Hutafika wewe mwenyewe au Wakili wako siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na Mahakama kama itakavyoamua pasipo wewe au Wakili wako kuwepo.
IMETOLEWA; kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama hii leo tarehe 15 mwezi wa Agosti,2023

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
DODOMA

---

***Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701***

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 0677020701**

**E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,**

**WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# ACT: BoT iingilie ununuzi mafuta

**Na Emmaloveness Gaston**

WAKATI Chama cha ACT-Wazalendo kikipendekeza serikali kurudisha ruzuku kwenye mafuta au Benki Kuu Tanzania (BoT) kuingilia ununuzi ili kukabiliana na mfumuko wa bei wa bidhaa hiyo, Chama cha Waagizaji na Wasambazaji wa Mafuta (TAOMAC), kimeomba kipewe fedha na serikali ili kinunue.

Aidha, kimesema kwa kuwa kuna tatizo la kupata dola, BoT iwalipe wauzaji kutoka nje moja kwa moja na kampuni za ndani ziilipie kwa Shilingi ya Tanzania.

Ushauri huo unakuja siku chache baada ya mfumuko wa bei ya mafuta unaochangiwa na uhaba wa Dola ya Marekani hali iliyosababisha mafuta kukosekana katika Bandari ya Mtwara na kupaa kwa bei hasa kwenye mikoa ya pembezoni.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Waziri Kivuli wa Nishati wa ACT-Wazalendo, Isihaka Mchinjita alisema, katika kukabiliana na bei ya mafuta wamependekeza mambo matano ambayo yakizingatiwa kutakuwa na ahueni.

"BoT inatakiwa kuwa mnunuzi mkuu wa bidhaa hiyo kwa kutafuta dola na kuwalipa wasambazaji wa nje ili iwe nafuu kwa ununuzi wa ndani kutumia shilingi kuilipa BoT kununua mafuta," alisema na kuongeza:

"Lakini pia kuondolewa kwa ruzuku kwenye bidha hiyo imesababisha kodi kuongezeka kwa Sh. 100 zaidi ambapo ni sawa na Sh. 450 ukilinganisha kabla ya ruzuku ilikuwa Sh. 350," alifafanua Mchinjita.

Vilevile, alipendekeza magari ya serikali na mabasi ya abiria ya mkoani kufungwa mfumo wa gesi ili kupunguza uhitaji wa mafuta na kutegemea dola katika kuagiza bidhaa hiyo.

"Kupunguza matumizi ya petroli na dizeli, magari ya serikali yafungwe mitambo ya gesi ili yatumie gesi ikiwa ni pamoja na magari ya mwendokasi, lengo kusaidia kupunguza gharama za uagizwaji wa mafuta pamoja na nauli nchini," alisema Mchinjita.

Kwa mujibu wa waziri kivuli huyo, ni vyema serikali ikaboresha miundombinu katika sekta ya utalii, ili idadi iongezeke na kuwa na uhakika wa upatikanaji wa dola na kuwa na akiba ya kutosha ya fedha hiyo.

**WAAGIZAJI/WACHUMI**

Mkurugenzi wa Chama cha Waagizaji na Wasambazaji wa Mafuta Tanzania (TAOMAC), Raphael Mgaya alisema kwa kuwa kampuni zinapata changamoto kupata dola, BoT iwalipe wauzaji kutoka nje kwa kutumia akiba ya dola waliyonayo.

"Kwa kuwa kampuni za mafuta zina uhaba wa dola kwa sasa serikali kupitia BoT iwalipe wasambazaji wa nje kutumia akiba yao wanunuzi wa ndani wanunue kwa BoT kwa kutumia shilingi," alibanisha.

Mchambuzi wa Uchumi, Walter Ngumi alisema ingawa ni kinyume cha sheria na sera kwa serikali kufanya biashara, haina budi kuwasaidia wananchi wake kupunguza gharama za mafuta ikizingatiwa akiba iliyopo ni kidogo.

"Tunachokitaka kwa serikali siyo kuwa wanunuzi 'direct' (moja kwa moja) wa mafuta kwa kuwa ilishawaachia kampuni binafsi ila tunacho kiomba wawapatie dola kampuni za mafuta ili zinunue na kuweka ruzuku katika bidhaa hiyo," alisema.

## Benki yakabidhi samani, mabati kwa shule 9 Ilala

**Na Maria Seme**

KATIKA jitihada za kuunga mkono mikakati ya serikali kutatua changamoto za sekta ya elimu, Benki ya NMB imekabidhi misaada ya viti na meza zake 134, madawati 200 na mabati 400 kwa shule tisa za msingi na sekondari wilayani Ilala, jijini Dar es Salaam, vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 51.3.

Ni sehemu ya utaratibu wa NMB kupitia Programu ya Uwajibikaji kwa Jamii (CSR), ambako kwa miaka minane sasa imekuwa ikitoa asilimia moja ya faida yake kwa jamii, kusaidia utatuzi wa changamoto.Mwaka huu imetenga zaidi ya Sh. bilioni 6.2.

Kwenye Viwanja vya Shule ya Msingi Mtakuja, iliyoko Vingunguti jijini. Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam, Dismas Prosper, alimkabidhi Mkuu wa Mkoa, Albert Chalamila, ambaye alikabidhi kwa Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogoro, aliyekabidhi pia kwa walimu na wakuu wa shule husika.

Prosper alisema madawati 200 vya Sh. milioni 20 yametolewa kwa Shule za Msingi Mtakuja, Miembeni, Vingunguti na Kombo, mabati 400 vya Sh. milioni 13.3 kwa Shule ya Msingi Airwing na Shule ya Sekondari Kerezange.

"Viti na meza zake 100 vya Sh. milioni 10 tunazitoa kwa Shule za Sekondari Kivule na Gerezani, viti na meza zake 34 vya Sh. milioni 8.3 vikiwa ni maalum kwa ajili ya walimu wa Shule ya Msingi Bonyokwa," alisema.

Chalamila aliishukuru NMB inavyotumia fungu la CSR kuunga mkono serikali kufanikisha mpango wa kutoa elimu bila malipo.



Ofisa Elimu wa Taaluma shule za msingi wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Nuru Kamota (kushoto), akizungumza na maofisa watendaji wa kata hivi karibuni, wakati wa mafunzo ya mpango wa shule salama kupinga ukatili wa kijinsia kwa wanafunzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

KESI DADA WA BILIONEA MSUYA

# Shahidi aonesha mahakama nguo ya ndani yenye damu

**Na Grace Gurisha**

SHAHIDI namba 16 katika kesi ya mauaji ya Aneth Msuya, Sajenti Elentruda (53), ameionesha mahakama matone ya damu ya tangu mwaka 2016 ambayo yalikuwa kwenye nguo ya ndani ya marehemu ambayo inadhaniwa alivuliwa kwa nguvu.

Aneth - mdogo wa mfanyabiashara wa madini mkoani Arusha, marehemu Erasto Msuya, maarufu Bilionea Msuya, aliuawa Mei 25, 2016 kwa kuchinjwa nyumbani kwake Kibada, Kigamboni, Dar es Salaam.

Askari huyo ambaye alikuwa Idara ya Uchunguzi wa Kisayansi ofisi ya RCO Temeke, aliionesha mahakama matone hayo jana mbele ya Jaji Edwin Kakolaki wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam wakati akiulizwa maswali ya dodoso na Wakili wa Utetezi, Peter Kibatala.

Wakili Kibatala alimtaka shahidi kutoa kielelezo cha ushahidi ndani ya bahasha ili aioneshe mahakama kama nguo hiyo ina damu na shahidi alitoa nguo hiyo akiwa amevaa mipira ya mkononi (gloves) na barakoa na kuionesha mahakama na wazee wa baraza.

Akionesha matone hayo akiwa ndani ya kizimba, Wakili Kibatala alichukua nguo hiyo ili kumwonesha kwa karibu Jaji na wazee wa mabaraza, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Yasinta Pater, alisimama na kuhoji anayetakiwa kuionesha mahakama ni shahidi au wakili.

"Hii haina shida akionesha shahidi au Kibatala haina shida, haya tuendelee na maswali," alisema Jaji Kakolaki.

Kibatala: Shahidi chukua kielelezo cha filimbi ya chuma ambayo ina rangi ya silver inadhaniwa kuwa ilikuwa inatumiwa na marehemu kwa maelezo yenu.

Shahidi alitoa filimbi kwenye bahasha na kuanza kuikagua.

**Kibatala: Je! Kwa mwonekano wa kawaida hiyo filimbi ina damu?**

**Shahidi:** Siwezi kuthibitisha kama ina damu kwa sababu mimi sio mtaalamu.

**Kibatala: Kama nilikusikia vizuri ulisema kwamba ulipokea vielelezo vitatu yaani chupi, filimbi na kisu kutoka kwa Sajenti John wa Kituo cha Polisi Kigamboni, Je! Kuna sehemu yoyote mliandikishana?**

**Shahidi:** Sisi tunafanya kazi ofisi moja, kwa hiyo tunagawana majukumu.

Akiendelea kujibu maswali ya dodoso ya wakili wa mshtakiwa wa pili, Nehemiah Nkoko, shahidi aliyakataa maelezo yake aliyoyatoa polisi kwa madai kuwa aliandika kwa mkono na hayo aliyopewa asome yamechapwa.

**Nkoko:** Mheshimiwa Jaji naomba nipewe maelezo halisi yaliyoandikwa kwa mkono na shahidi na kama hawana basi nitaomba nitumie yaliyochapwa.

Jaji: Nawauliza hayo maelezo yapo kama yapo apewe

**Peter:** Mheshimiwa Jaji hatuna hayo maelezo, tunayo ambayo yamechapwa, halisi yatakuwa ofisini.

**Nkoko:** Kwa hiyo nitumie haya ambayo yamechapwa?

**Peter:** Ni sawa hatuna pingamizi.

Shahidi alipopewa maelezo hayo asome ili aulizwe maswali, alipoona mambo ni tofauti na kile ambacho alikieleza mbele ya mahakama alidai kuwa ni typing error (makosa kiuchapaji) na kwamba maelezo hayo hayatambui na hajui yametolewa wapi.

Hali hiyo ilisababisha, wakili Nkoko kuiomba mahakama iweke kwenye rekodi tofauti zilizoonekana na pia kuiomba mahakama ipokee maelezo ya shahidi huyo yaliyochapwa kwa sababu anazungumza uongo.

Awali, akisoma maelezo hayo kimya kimya, alidai kuwa hayo ni maelezo yake aliyoandika, lakini baadae alibadilisha kuwa hayatambui baada ya wakili Nkoko kumueleza kwamba maelezo yake ya mahakamani na aliyoandika yanatofautiana, kwa hiyo aliidanganya mahakama.

"Mimi siyatambui haya maelezo, nayatambua niliyoandika kwa mkono wangu mwenyewe sasa haya sijui wameyatoa wapi kwa sababu yana mapungufu sana, niulizwe maswali kwa maelezo niliyoandika kwa mkono," alidai shahidi.

Wakili Peter, alipinga kupokewa kwa maelekezo hayo kwa madai kuwa aliyepaswa kuiomba mahakama ni shahidi mwenyewe na pia kisheria mahakama haiwezi kupokea nakala, kielelezo ambacho hakijakidhi matakwa ya kisheria.

Washitakiwa katika kesi hiyo ni mke wa aliyekuwa mfanyabiashara wa madini, marehemu Erasto Msuya, Miriam Mrita na mfanyabiashara Revocatus Muyela, wote wakazi wa Arusha.

# FEI TOTO AVUNJA REKODI, KITAYOSCE 'KUNAFUKUTA'

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

KIUNGO mpya wa Azam FC, Feisal Salum 'Fei Toto' ameweka rekodi ya kufunga hat-trick ndani ya dakika 12 waliivaa Kitayosce katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi usiku huku ikizua mjadala mkubwa.

**Mpaka mwamuzi wa mechi hiyo, Omari Mdoe, kutoka Tanga anapuliza filimbi kumaliza mchezo, Azam ilikuwa inaongoza kwa mabao 4-0, moja likifungwa na Prince Dube.**

Inakuwa ni 'hat-trick' ya muda mfupi zaidi kwenye historia ya Ligi Kuu Tanzania Bara, ikivunja iliyowekwa wa straika wa Simba, Mkongomani Jean Baleke aliyoiweka msimu uliopita.

Baleke alitumia dakika 34 kupata hat-trick ambayo ilisimama ndiyo ya muda mfupi zaidi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Wakata Baleke akifunga dakika ya tatu, saba na 34, juzi Fei Toto alifunga dakika ya tatu, tisa na 12.

Fei Toto pia ameweka rekodi ya kuwa mchezaji aliyefunga bao la kwanza la msimu huu kwenye timu yake.

Hata hivyo, mechi hiyo ilivunjika baada ya wachezaji wa Kitayosce kuwa pungufu ya wachezaji saba.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kitayosce, Thabit Kandoro, alisema tatizo lililojitokeza ni kushindwa kupatikana vibali vya kazi kwa wachezaji wa kigeni, huku wawili wa Kitanzania waliokuwa usajili wako haukukamilika.



"Tuna wachezaji 27, tumekuja Dar na wachezaji 20, 10 wageni na 10 ni Watanzania, kilichotokea ni hawa wageni wamekosa vibali vya kufanya kazi, na wawili wa Kitanzania wana matatizo kwenye usajili, pamoja na hayo wachezaji waliocheza kabla ya mechi walikuwa na malaria," alisema Kandoro.

Hata hivyo alisema mamlaka ingeweza kuwaruhusu kuwatumia kwa sababu wachezaji wote wageni wana viza ya kibiashara ambayo inawaruhusu kufanya kazi kwa miezi mitatu wakati suala likishughulikiwa.

Naye Ofisa Habari wa Bodi ya Ligi, Karim Boimanda, alisema mabao yaliyofungwa na wachezaji wa Azam FC yanatambulika kwa mujibu wa kanuni.

Wakati huo huo, Kocha Mkuu wa Kitayosce, Goran Kopunovic, ameweka wazi hatarejea Tabora hadi atakapomalizana na uongozi wa timu hiyo.

Kopunovic aliliambia Nipashe viongozi wa timu hiyo iliyopanda daraja wamekuwa na shida katika kukamilisha usajili pamoja na mambo mengine ya kiutendaji ambayo amewataka kuyakamilisha mapema.



Kiungo wa JKT Queens, Esther Mabanza (katikati), akijipanga kuwatoa wachezaji wa New Generation ya Zanzibar katika mechi ya mashindano ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA) iliyochezwa kwenye Uwanja wa Lugogo jijini Kampala, Uganda juzi. JKT Queens ilishinda bao 1-0. **PICHA: CECAFA**

# Azam FC yaenda Ethiopia kibabe

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuanza vizuri msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara, kikosi cha Azam FC kimeondoka nchini jana usiku kuelekea Ethiopia kikiwa na matumaini ya kufanya vyema katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Azam itacheza mechi ya kwanza dhidi ya wenyeji Bahir Dar Kenema utakaofanyika kesho huku marudiano yakiwa ni Agosti 25, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex,Dar es Salaam.

Ofisa Habari wa Azam FC, Hashim Ibwe, alisema mechi dhidi ya Kitayosce haikuwa kipimo kizuri kwao kuelekea mchezo wa kimataifa kwa sababu hawakupata ushindani mkubwa.

Hata hivyo Ibwe alisema wachezaji wao wako tayari kwa ajili ya mchezo huo kwa kimataifa na wanakwenda kupambana kuhakikisha wanapata matokeo mazuri.

"Tunaondoka leo (jana) usiku kuelekea Ethiopia, huko tunaenda kupambana kusaka ushindi, hautakuwa mchezo rahisi kwa sababu timu yeyote iliyofanikiwa kushiriki michuano hii ni wazi wako vizuri," alisema Ibwe.

Aliongeza kocha wao (Youssouph Dabo) anatumia madhaifu ya kikosi chake aliyoyaona katika michuano ya Ngao ya Jamii kurekebisha katika kila eneo ili kufanya vizuri katika mchezo huo wa kimataifa.

Aliongeza malengo ya Azam msimu huu ni kufika mbali katika michuano hiyo kwa kuanza na kupata ushindi ugenini.

## TFF, TAKUKURU kushirikiana Bara

**Na Saada Akida**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF) na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Nchini (TAKUKURU) wameungana kwa ajili ya kutoa elimu kwa wanamichezo ili kushiriki kutoa taarifa zinazoashiria rushwa michezoni.

Akizungumza jijini jana, Mkurugenzi wa Sheria, Habari na Masoko wa TFF, Boniface Wambura, alisema uamuzi wa kushirikiana na taasisi umetokana na kuwapo kwa changamoto ya masuala ya rushwa katika soka hapa nchini.

Wambura alisema wamejipanga kutoa elimu kwa wanamichezo kwa ajili ya kuwaeleza juu ya athari za kutoa au kupokea rushwa na jinsi ya kufikisha taarifa hizo katika mamlaka husika.

Naye Mkurugenzi wa Elimu kwa Umma wa TAKUKURU, Joseph Mwaiswelo, alisema lengo la kuungana na TFF ni kuimarisha furaha kupitia mpira wa miguu kwa sababu rushwa ni adui mkubwa kwa taifa la Tanzania.

"Katika michezo kuna tuhuma nyingi sana, tumelazimika kuingia katika soka ili kuelimusha jamii kupinga suala la rushwa na kujenga ujasili kwa wadau wa michezo ili kufanya mchezo huu kuwa wa kiungwana," alisema Mwaiswelo.

## Singida FG, JKU majaribuni CAF

**Na Saada Akida**

SINGIDA Fountain Gate inatarajia kuivaa JKU FC kutoka Zanzibar katika mchezo wa awali wa mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Kocha Mkuu wa Singida Fountain Gate, Hans van der Pluijm, alisema wamejiandaa vizuri kwa kufanyia kazi mapungufu aliyoyaona katika michuano ya Ngao ya Jamii iliyomalizika Jumapili iliyopita jijini Tanga.



Pluijm alisema wachezaji wake wako tayari kusaka ushindi na kujiweka katika nafasi nzuri ya kusonga mbele na anatambua mchezo huo utakuwa na ushindani mkubwa kwa sababu ya wapinzani pia wamejiandaa vizuri.

"Tumefanyia kazi mapungufu yetu yaliyojitikeza Tanga, sasa kikosi kipo tayari katika mchezo wetu wa kwanza wa michuano hii ya kimataifa dhidi ya JKU FC, tutapambana ili kupata matokeo mazuri," alisema Pluijm.

Kocha Msaidizi wa JKU, Salum Ally, alisema wamejiandaa vizuri kuwakabili wapinzani wao baada ya kuweka kambi maalumu ya muda wa wiki tatu hapa Dar es Salaam.

## ZISIKUPITE

### DOUCOURE ATAKIWA LIVER

KLABU ya Liverpool imeongeza juhudi zake za kumsajili kiungo wa kati wa Crystal Palace na Timu ya Taifa ya Mali, Cheick Doucoure mwenye umri wa miaka 23. ***(Independent)***

### LIVERPOOL KUMNASA ENDO

LIVERPOOL pia inatarajiwa kulipa euro milioni 19 kwa kiungo wa Stuttgart na Timu ya Taifa ya Japan, Wataru Endo, mwenye umri wa miaka 30. ***(Athletic)***

### LINGARD ANUKIA WEST HAM

KLABU ya West Ham inatathmini uwezekano wa kumsajili kiungo wa zamani wa England, Jesse Lingard, mwenye umri wa miaka 30, ambaye ni mchezaji huru baada ya kuachiwa na Nottingham Forest kutokana na mkataba wake kumalizika. ***(Sky Sports, via Football Daily)***

### SILVA MAMBO MAZURI

KIUNGO wa kati wa Timu ya Ureno, Bernardo Silva, mwenye umri wa miaka 29 ataongeza mkataba wake Manchester City kwa kitita cha euro milioni 50 msimu huu. ***(El Chiringuito TV)***

### CHELSEA KUMUUZA HALL

CHELSEA imemweka sokoni kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya England ya vijana wa umri chini ya miaka 21, Lewis Hall (18). ***(Telegraph)***

### MITROVIC KUELEKEA SAUDIA

KLABU ya Saudi Arabia Al-Hilal inakaribia kufikia makubaliano ya kumsajili, Aleksandar Mitrovic, mwenye umri wa miaka 28 kutoka Fulham baada ya kurejesha nia yao ya kumnunua mshambuliaji huyo wa Serbia. ***(Guardian)***

### WAHI SOKONI ENGLAND

KLABU ya West Ham inavutiwa na mshambuliaji wa Montpellier, Elye Wahi, mwenye umri wa miaka 20. ***(Guardian)***

### FATI AGOMBEWA EPL

MSHAMBULIAJI wa Hispania, Ansu Fati, mwenye umri wa miaka 20, ameripotiwa kuchagua kuondoka Barcelona, huku Manchester United, Arsenal na Tottenham Hotspur zikiwa miongoni mwa klabu za Ligi Kuu England zinazomwania. ***(AS)***

### BAILLY KUONDOKA UNITED

MLINZI wa Ivory Coast, Eric Bailly, 29 na Manchester United wamefikia makubaliano ya mchezaji huyo kuondoka katika klabu hiyo bure msimu huu wa joto, huku Fulham wakiripotiwa kumtaka. ***(RMC Sport)***

### DE GEA AITAKA BAYERN

GOLIKIPA wa Hispania ambaye ni mchezaji huru, David de Gea, mwenye umri wa miaka 32, anatamani kuhamia Bayern Munich baada ya kuondoka Manchester United msimu huu. ***(Mirror)***

### ALEMANY KUTUA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inamfikiria, Mateu Alemany, ambaye ataondoka Barcelona mwezi ujao kama chaguo linalowezekana kwa mkurugenzi wao mpya wa soka. ***(Fabrizio Romano)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# GRIEZMANN: NITAMFUATA MESSI MIAMI MAREKANI

**Mfaransa huyo naye anahitaji kuweka historia nyingine...**

**MADRID,** Hispania

ANTOINE Griezmann amekiri anafuatilia ushujaa wa "ajabu" wa Lionel Messi kule Inter Miami, huku fowadi huyo wa Atletico Madrid akisema bado ana matumaini ya kumalizia soka lake kwa kucheza Ligi Kuu ya Marekani (MLS).

**Messi mwenye umri wa miaka 36, amefunga katika mechi zake zote za Inter Miami hadi sasa akiwa amefunga mabao tisa kwenye mechi sita, ikiwa ni pamoja na ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Philadelphia Union hapo Jumanne na kutinga fainali ya Kombe la Ligi.**

Griezmann, mchezaji mwenzake wa zamani na Messi katika kikosi cha Barcelona anavutiwa kwa muda mrefu na michezo na utamaduni wa Marekani na hajaweka siri ya kutaka kufurahia maisha ya MLS katika siku zijazo.

"Ndio, namfuata Messi," alisema Griezmann akiwaambia waandishi wa habari.

"Leo ndiye bora katika historia, anajaza viwanja, anafunga mabao mengi na anashinda michezo.

"Yeye ni mzuri na nadhani ni jambo bora zaidi ambalo MLS wamefanya kumchukua leo, katika suala la uuzaji na mpira wa miguu."

Griezmann (32), alikuwa mmoja wa wachezaji bora wa LaLiga msimu uliopita, akifunga mabao 15 na kutoa pasi za mabao 16 za juu kwenye ligi huku Atletico Madrid wakimaliza nafasi ya tatu nyuma ya Barcelona na Real Madrid.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa alisema bado anatumaini "kuweka historia" huko Atletico lakini yuko wazi kuhusu kutaka kujaribu bahati yake Marekani.

"Siku zote nimesema," alisema Griezmann.

"Lengo langu ni kuishia hapo, na kila kitu ninachopenda kuhusu michezo ya Marekani, kucheza kwenye MLS na kufurahia, kuweza kushinda vitu na kuwa katika kiwango changu bora.

"Kwanza nataka kuweka historia hapa na kushinda mataji pale Atletico. Baada ya hapo tutaona... nadhani uwepo Leo, Sergio Busquets na Jordi Alba ni mzuri kwa ligi. . Hilo na kusajili wachezaji wachanga, hasa kutoka Amerika Kusini, ni jambo bora zaidi ligi inaweza kufanya."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,144,1

MECHI KALI
WERDER BREMEN
VERSUS
BAYERN MUNCHEN
1 | 7.70
X | 5.83
2 | 1.34

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# NEYMAR AFURAHIA KUWA NA RONALDO, BENZEMA SAUDIA



**RIYADH,** Saudi Arabia

NEYMAR amesema amehamia ligi "yenye ushindani mkubwa" kwa kujiunga na Al Hilal ya Saudi Arabia na kumsifu, Cristiano Ronaldo kwa ushawishi licha ya kuitwa "kichaa" alipohamia Mashariki ya Kati hapo Desemba, mwaka jana.

Mshambuliaji huyo wa Brazil, Neymar (31), aliwaacha mabingwa wa Ufaransa Paris Saint-Germain na kujiunga na Al Hilal yenye makao yake Riyadh, mabingwa watetezi wa bara la Asia, kwa uhamisho wa thamani ya dola milioni 98.6.

Nyota huyo wa zamani wa Barcelona alikuwa akihusishwa na kuhamia Manchester United, Chelsea au kurejea Camp Nou msimu huu wa joto, lakini akaamua kujiunga na Al Hilal.

"Ninaamini Cristiano Ronaldo alianzisha haya yote na kila mtu alimwita 'kichaa,' na hivi na vile," alisema Neymar. Leo unaona ligi inakua zaidi na zaidi.

"Ligi itakuwa na ushindani mkubwa hasa baada ya usajili uliofanyika kwenye dirisha la usajili la majira ya joto, naamini ushindani ni muhimu ndiyo maana najiunga na ligi hii, ninasukumwa na changamoto, nipo kusaidia ligi kukua.

"Nina furaha sana kuandika historia mpya ya kufuatilia malengo yote na klabu na wachezaji wenzangu, kushinda mataji zaidi na zaidi na kutimiza azma ya klabu."

Neymar, ambaye anaripotiwa atakuwa akipokea mshahara wa kila mwaka wa dola milioni 10 katika klabu ya Al Hilal, anafanya idadi ya uhamisho kwenda Saudi Arabia kutoka Ligi Kuu za Ulaya (England, Ufaransa, Hispania, Italia, Ujerumani na Ureno) kufikia zaidi ya 30.



# Timber aipa pigo Arsena

**LONDON,** England

KLABU ya Arsenal imethibitisha, Jurrien Timber alipata jeraha kwenye goti wakati wa ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Nottingham Forest katika mechi iliyochezwa Jumamosi iliyopita na atahitaji kufanyiwa upasuaji.

Beki huyo, ambaye alijiunga na Arsenal msimu huu wa joto akitokea Ajax, alianza kwa mara ya kwanza katika Ligi Kuu England, lakini ilibidi aondolewe baada ya muda wa mapumziko.

"Zaidi ya tathmini za kina na madaktari tangu Jumamosi, tunathibitisha Jurrien Timber amepata jeraha kwenye goti lake la kulia," ilisema taarifa.

"Usaidizi na utaalamu kutoka kwa timu yetu ya matibabu na kila mtu katika klabu sasa utaelekezwa kwenye mpango wa kumsaidia Jurrien, ili kuhakikisha anapona
zuri na anarejea kuch
haraka iwezekanavyo

Akitumia mtandao
kijamii, Timber m
nyewe alisema: "Jer
langu ni baya zaidi
liko ilivyotarajiwa,
wa baada ya mapo
mazuri niliyopoke
Nilitaka kukulipa uw
jani, jambo amb
halitawezekana kwa
indi kijacho. Asante
kunifanya nijisikie ny
bani."

72,464/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 19/08/23 | 17:00 | Fulham FC vs Brentford FC | 2.55 | 3.25 | 2.60 |
| 02. 19/08/23 | 19:15 | Caykur Rizespor vs Alanyaspor | 2.36 | 3.25 | 2.55 |
| 03. 19/08/23 | 19:30 | Tottenham Hotspur vs Manchester United | 3.00 | 3.40 | 2.21 |
| 04. 19/08/23 | 19:30 | Empoli FC vs Hellas Verona | 2.35 | 3.15 | 2.95 |
| 05. 19/08/23 | 21:45 | Hatayspor Antakya vs Kasimpasa Istanbul | 2.32 | 3.35 | 2.60 |
| 06. 19/08/23 | 21:45 | Genoa CFC vs ACF Fiorentina | 2.95 | 3.25 | 2.30 |
| 07. 19/08/23 | 22:30 | Portimonense SC vs Boavista Porto | 2.43 | 3.10 | 2.90 |
| 08. 19/08/23 | 22:30 | CA Osasuna vs Athletic Bilbao | 2.75 | 3.05 | 2.60 |
| 09. 20/08/23 | 14:30 | VfL 1899 Osnabruck vs FC Nuremberg | 2.48 | 3.40 | 2.60 |
| 10. 20/08/23 | 14:30 | Holstein Kiel vs FC Magdeburg | 2.35 | 3.55 | 2.70 |
| 11. 20/08/23 | 16:00 | Le Havre AC vs Stade Brest 29 | 2.55 | 3.20 | 2.65 |
| 12. 20/08/23 | 16:00 | FC Lorient vs OGC Nice | 3.05 | 3.40 | 2.18 |
| 13. 20/08/23 | 17:30 | Estoril Praia vs Rio Ave FC | 2.40 | 3.15 | 2.90 |
| 14. 20/08/23 | 18:00 | Hamarkameratene vs Rosenborg BK | 2.70 | 3.25 | 2.26 |
| 15. 20/08/23 | 19:00 | FC Sudtirol Bolzano vs Spezia Calcio | 3.15 | 2.95 | 2.15 |
| 16. 20/08/23 | 20:15 | KV Kortrijk vs KAS Eupen | 2.15 | 3.45 | 3.10 |
| 17. 20/08/23 | 21:45 | RC Lens vs Stade Rennes | 2.33 | 3.50 | 2.75 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 18/08/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 5944 | Avispa Fukuoka vs Niigata Albirex | 1.84 | 3.23 | 3.88 |
| 13:30 | 2637 | Suwon Samsung vs Jeju Utd | 2.63 | 3.03 | 2.50 |
| 13:30 | 4809 | Incheon Utd vs Gwangju | 2.50 | 2.98 | 2.67 |
| 14:35 | 2013 | Shandong Luneng vs Tianjin Teda | 1.28 | 4.85 | 8.08 |
| 14:35 | 2588 | Hangzhou NG vs Qingdao Hainiu | 1.80 | 3.54 | 3.69 |
| 14:35 | 4537 | Shanghai SIPG vs Meizhou Kejia | 1.20 | 5.68 | 10.14 |
| 15:00 | 1036 | Persita Tangerang vs PSS Sleman | 1.74 | 3.53 | 3.99 |
| 17:00 | 1165 | Ittihad Kalba vs Al Sharjah SC | 3.78 | 3.43 | 1.81 |
| 18:00 | 2114 | Artsakh vs Shirak Gyumri | 2.28 | 3.10 | 2.95 |
| 18:00 | 3158 | Lahti vs VPS Vaasa | 2.78 | 3.23 | 2.27 |
| 18:00 | 3891 | AL Akhdood vs Al Fateh (KSA) | 3.35 | 3.51 | 2.05 |
| 18:30 | 1960 | IFK Mariehamn vs Honka | 2.92 | 3.18 | 2.21 |
| 18:30 | 5825 | Al Ahli Doha SC vs Lekhwiya SC | 8.69 | 5.25 | 1.24 |
| 18:45 | 1290 | Sparta Prague B vs Zbrojovka Brno | 2.98 | 3.28 | 2.13 |
| 19:00 | 1221 | Puskas Akademia vs Videoton FC | 1.84 | 3.31 | 3.92 |
| 19:00 | 1223 | Zorya Lugansk vs Oleksandria | 2.57 | 3.18 | 2.46 |
| 19:00 | 1531 | FK Imt Novi Beograd vs Cukaricki St | 3.24 | 3.29 | 2.01 |
| 19:30 | 2540 | Al Ain vs Baniyas | 1.18 | 5.84 | 11.08 |
| 19:30 | 3248 | Kaiserslautern vs SV Elversberg | 2.14 | 3.50 | 3.05 |
| 19:30 | 4168 | Wehen vs Karlsruher SC | 3.15 | 3.60 | 2.06 |
| 20:00 | 3693 | FC Andorra vs FC Cartagena | 1.90 | 3.32 | 3.81 |
| 20:00 | 4441 | Hvidovre IF vs Copenhagen | 6.45 | 4.43 | 1.44 |
| 20:30 | 1995 | Umm-Salal SC vs Al Sadd SC | 6.48 | 4.96 | 1.33 |
| 20:30 | 2163 | SuperSport Utd vs Cape Town City | 2.04 | 3.08 | 3.64 |
| 20:30 | 3855 | Mallorca vs Villarreal | 2.94 | 3.14 | 2.56 |
| 20:30 | 5457 | Bloemfontein Celtic vs Stellenbosch | 2.45 | 3.07 | 2.81 |
| 21:00 | 1101 | FC Oss vs Jong PSV | 2.66 | 3.32 | 2.39 |
| 21:00 | 1310 | Istanbulspor vs Kayserispor | 2.35 | 3.50 | 2.68 |
| 21:00 | 1472 | Heracles Almelo vs NEC Nijmegen | 2.35 | 3.36 | 2.72 |
| 21:00 | 1753 | NAC Breda vs Jong AZ Alkmaar | 1.82 | 3.62 | 3.72 |
| 21:00 | 2187 | Volos vs Lamia | 2.47 | 3.24 | 2.77 |
| 21:00 | 2747 | Al Nasr Riyadh vs Al Taawon | 1.55 | 3.91 | 5.84 |
| 21:00 | 3118 | Emmen vs VVV Venlo | 1.77 | 3.64 | 3.90 |
| 21:00 | 3387 | Telstar vs Cambuur | 3.27 | 3.27 | 2.07 |
| 21:00 | 3762 | Al Wehda vs Al Shabab Riyadh | 2.99 | 3.20 | 2.37 |
| 21:00 | 3889 | Helmond Sport vs Den Bosch | 2.01 | 3.42 | 3.27 |
| 21:00 | 5143 | Antalyaspor vs Konyaspor | 2.31 | 3.41 | 2.79 |
| 21:00 | 5433 | AL Hazm vs Al-Ettifaq | 3.20 | 3.20 | 2.25 |
| 21:30 | 2289 | Bari vs Palermo | 2.33 | 3.13 | 2.93 |
| 21:30 | 5351 | Werder Bremen vs Bayern Munchen | 7.70 | 5.83 | 1.34 |
| 21:45 | 1954 | Ballymena Utd vs Linfield Belfast | 6.05 | 4.33 | 1.40 |
| 21:45 | 3892 | Cork City vs Waterford Utd | 2.41 | 3.26 | 2.65 |
| 21:45 | 5782 | Kerry FC vs Drogheda Utd | 9.55 | 6.50 | 1.19 |
| 21:45 | 5798 | Nottingham vs Sheffield Utd | 2.31 | 3.34 | 3.14 |
| 22:00 | 1251 | Leeds vs West Bromwich | 1.79 | 3.42 | 4.16 |
| 22:00 | 2515 | Metz vs Marseille | 4.62 | 4.05 | 1.70 |
| 22:15 | 1552 | Casa Pia Atletico vs Sporting Lisbon | 6.77 | 4.08 | 1.44 |
| 22:30 | 3555 | Zaragoza vs Valladolid | 2.47 | 2.97 | 2.87 |
| 22:30 | 4161 | Defensa Justicia vs Godoy Cruz | 2.07 | 3.10 | 3.41 |
| 22:30 | 5541 | Valencia vs Las Palmas UD | 1.80 | 3.49 | 4.83 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# BOSI WA WAAMUZI AKEMEA WACHEZAJI KUTISHA MAREFA

INATOKA UKURASA 24

"Zamani waamuzi wengi walikuwa na umri mkubwa, mchezaji anamwamkia mwamuzi. Kwa bahati nzuri mimi ndiye niliyeleta mabadiliko kwa kuanza uamuzi nikiwa kijana sana kiasi kwamba mimi ndiye niliyekuwa ninawaamkia wachezaji," alisema.

Hamduni anayetajwa kuwa mwamuzi bora zaidi kihistoria nchini, alisema pamoja na hayo, heshima ilipewa kipaumbele, licha ya kuwapo changamoto za hapa na pale kwa baadhi ya wachezaji wakorofi.

"Mimi pia nilishawahi kukumbana na wachezaji wakorofi, lakini nilikuwa ninaonesha mamlaka yangu uwanjani kwa kusimamia sheria. Kosa lolote la kimchezo hakuna kusita kulitolea adhabu ikiwamo kadi nilizokuwa nazo," alisema.

Mkongwe huyo katika faini ya uamuzi wa mpira wa miguu, aliwahakikishia wadau wa mchezo huo ataendelea kuwa mkali kwa waamuzi watakaovurunda kama ilivyokuwa msimu uliopita ambao zaidi ya waamuzi 10 walisimamishwa.

"Kutokana na malalamiko mengi kutoka kwa wadau wa soka, sisi Kamati wa Waamuzi tunawaambia waamuzi wetu wahakikishe sheria 17 zisimamiwa kwenye Ligi Kuu. Kujiandaa kwetu zaidi tumewapa mafunzo mazuri ambayo tunahakikisha kama wameiva kwa ajili ya kusimamisha sheria zote za soka.

"Tumehakikisha waamuzi wote wanafanya vyema kwenye mtihani wa utimamu wa mwili kwa waamuzi wote 600 wanachezesha ligi zote nchini, na ili acheze ni lazima ashinde na kama wakishindwa hasa kwa waamuzi wale wa FIFA, huwa wanarudia tena awamu ya pili.

"Hatutaki wafanye makosa. Timu zimejiandaa, wadau wa soka wamejiandaa na sisi kama Kamati ya Waamuzi tunayapokea na kuyafanyia kazi malalamiko yanayojitokeza na mara nyingi tunaangalia matukio ya mechi za msimu uliopita na kuwa somo kwa ajili ya kuwafanya wawe bora msimu huu. Tunaomba wadau wa soka watuamini katika jambo hili," alisema.




Mwenyekiti wa Kamati ya Waamuzi ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Nassor Hamduni. **PICHA: MTANDAO**

# Simba yaanza na 4G



INATOKA UKURASA 24

zania Bara ikiwa nyuma ya Azam FC ambayo juzi iliikung'uta Kitayosce mabao 4-0.

Mabao mawili iliyofungwa Simba jana ndiyo yanawafanya kuwa nyuma ya vinara Azam inayoongoza kabla ya mechi zingine za raundi ya kwanza kuchezwa.

Goli la jana la Baleke limemfanya Mkongomani huyo kuwa amefunga bao katika mechi za mwisho Simba ilipokutana na Mtibwa Sugar.

Baleke alifunga 'hattrick' kwenye mchezo wa mwisho timu hizo zilipokutana kwenye ligi msimu uliopita Machi 11 mwaka huu ambapo Simba ilishinda mabao 3-0.


Katika mchezo wa jana, Simba ilifanya mabadiliko kadhaa ambapo kwa nyakati tofauti walitoka Onana Kanoute nafasi zao zikachukuliwa na Saido Ntibazonkiza na Mzamiru Yassin, huku pia wakitoka Baleke na Kennedy nafasi zao zikachukuliwa na Moses Phiri na Hussein Kazi.

Mabadiliko hayo kwa kiasi kikubwa yaliisaidia Simba kuibuka na ushindi huo muhimu.

Michezo

Ijumaa Agosti 18, 2023

Nipashe



Timber aipa pigo Arsenal UKURASA 22



Golikipa wa Mtibwa Sugar, Mohamed Makaka (kushoto) akiruka bila mafanikio kuzuia mpira wa kichwa uliopigwa na mshambuliaji wa Simba, Essomba Onana (wa pili Kulia) kwenye mchezo wa ligi kuu Tanzania Bara jana kwenye uwanja wa Manungu Complex mkoani Morogoro, Simba ilishinda 4-2. **PICHA: MTANDAO**

# Simba yaanza na 4G

## Robertinho amlilia Inonga, safu ya ulinzi ikiruhusu mabao mawili ndani ya dakika mbili...

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya Simba kuanza kwa ushindi wa '4G' baada ya kuifunga Mtibwa Sugar mabao 4-2 kwenye mchezo wao wa kwanza wa ligi kuu Tanzania Bara msimu wa 2023/2024, Kocha Roberto Oliviera, amesema kukosekana kwa beki wake wa kati Henock Inonga kumechangia kufungwa mabao mawili ya haraka haraka kwenye mchezo huo uliochezwa uwanja wa Manungu Complex mkoani Morogoro.

**Jana Simba ikiwa mbele kwa mabao 2-0 mpaka dakika ya 10 ya kipindi cha kwanza, Mtibwa Sugar iliwashangaza kwa kusawazisha mabao hayo ndani ya dakika mbili.**

Baada ya magoli ya Jean Baleke aliyefunga katika dakika ya tano tu ya mchezo akiunganisha krosi ya Kibu Denis na bao la Essomba Onana katika dakika ya tisa, mshambuliaji wa Mtibwa Sugar Matheo Anthon alisawazisha mabao hayo katika dakika za 20 na 22 akitumia makosa ya safu ya ulinzi ya Simba iliyokuwa chini ya Che Malone na Kennedy Juma kama mabeki wa kati na pembeni wakicheza Mohamed Hussein na Shomari Kapombe ambao walionekana kutoelewana hasa kipindi hiko cha kwanza.

Hata hivyo ikiwa imebaki dakika moja kwenda mapumziko, Patrice Ngoma aliipatia Simba bao la tatu akiunganisha kwa kichwa mpira uliotoka kwa Clatous Chama na kumpoteza golikipa wa Mtibwa Sugar Mohamed Makaka.

"Nashukuru kupata ushindi huu muhimu tukiwa ugenini, lakini lazima niseme wazi leo (jana) kukosekana kwa Inonga bado kunatugharimu kwenye safu ya ulinzi, kwangu mimi ni beki bora sana, nalazimika kuanza na Kenedy kucheza na Che Malone, bado hawajaelewana sana, lakini kikubwa ni ushindi kwa sababu si kitu chepesi kupata ushindi ugenini," alisema Robertinho.

Alisema taratibu timu yake inazidi kuimarika kwa wachezaji kuelewana na anaamini mashabiki na wapenzi watafurahia soka safi la timu yake.

Katika mchezo huo wa jana ulioanza taratibu kwa timu zote mpaka kipindi cha kwanza kinakamilika Simba ilikuwa mbele kwa mabao hayo zilikuwa zimefungana mabao hayo 3-2.

Kipindi cha pili Simba walianza mchezo huo kwa kasi wakicheza soka la pasi fupi fupi na kufanikiwa kupata bao la nne kupitia kwa Chama aliyepokea pasi safi ya Luis Miquissone aliyeingia kipindi cha pili kuchukua nafasi ya Baleke.

Ushindi wa jana unawapeleka Simba kwenye nafasi ya pili ya msimamo wa Ligi Kuu Tan-

INAENDELEA UKURASA 23

## Bosi wa waamuzi akemea wachezaji kutisha marefa

**Na Adam Fungamwango**

MWENYEKITI wa Kamati ya Waamuzi ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Nassor Hamduni, amekemea tabia anayoitaja imejitokeza hivi karibuni ya baadhi ya wachezaji kuwazingira, kuwakemea na kuwatisha waamuzi uwanjani, hasa wa kike.

Katika mazungumzo mahususi na Nipashe katika Uwanja wa Mkapa, Dar es Salaam mwanzoni mwa wiki, Hamduni, mwamuzi wa zamani wa kimataifa, alisema kuwa baadhi ya wachezaji wameonekana kuwa na utovu wa nidhamu kwa waamuzi, hasa wa kike, kwa kupinga uamuzi wao na kuonekana kuwatolea maneno yasiyofaa.

"Hii si vizuri hata kidogo! Na kwa sababu inaonekana kwenye televisheni, wengine wakiona wanaendelea na tabia hii.

"Ninawapongeza sana waamuzi wetu kwa sababu nao hawaingii kwenye jazba ya wachezaji badala yake wanafuata sheria na kanuni inavyomwelekeza, vinginevyo kama na wao wangekuwa wanajibu mapigo, na wao ndiyo wanaoamua kila kitu uwanjani, sidhani kama hali ingekuwa nzuri," alionya.

Alisema ameona baadhi ya mechi wachezaji wakiwazonga waamuzi wa kike, akitoa mfano mechi ya Ngao ya Jamii kati ya Singida Fountaine Gate dhidi ya Simba - aliona baadhi ya wachezaji walikuwa wanamsumbua mwamuzi Amina Kyando.

"Waamuzi wetu wanatumia busara sana kwa sababu nchi zingine huwezi kumzonga, kumshika, wala kumzunguka mwamuzi ukimfokea. Hili jambo mimi ninaomba wale wachezaji wenye tabia hiyo waache kwa sababu yeye akishatoa uamuzi, hata ufanye nini hawezi kubadilisha," alisisitiza.

**SHIKAMOO!**

Hamduni alisema wachezaji wa sasa wanapata bahati ya kuchezeshwa na waamuzi vijana, hivyo wawe na nidhamu na upendo kwao kwa kuwa zamani wachezaji wengi walikuwa wakichezeshwa na waamuzi wenye umri mkubwa sawa na baba zao.

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >